

# Juu ya Mbawa Za Hua Mweupe Kama Theluji

Shreveport, Louisiana USA

Novemba 28, 1965J

1 Na tuinamishe vichwa vyetu.

Mpendwa Bwana, tunakushukuru usiku wa leo kwa ajili ya ahadi ya kuja kwa Bwana Yesu, ambapo tutakutana katika mkutano mkuu ambapo hautakwisha kamwe, wa furaha na nyimbo, tunapokusifu katika —katika nyakati zisizo na mwisho zijazo. Tunaomba baraka Zako kwenye mkutano usiku wa leo. Tunaomba baraka Zako juu ya maskani hii, juu ya watumishi wake, wachungaji wake, watenda kazi pamoja nayo, wachungaji wenza, na wengine wote.

Tunakuomba uwabariki hawa, Bwana, ambao wamekuja maili nyingi kuja mkutanoni, weka mkono Wako wa rehema juu yao wanaposafiri kurudi makwao. Tujalie, Bwana. Jalia tukutane mara nyingi zaidi pamoja mahali hapa panapoitwa nyumba ya Mungu, kuabudu. Wabariki wale wanaosikiliza usiku wa leo, Bwana, kwa njia ya simu. Jalia kila mtu asiyeokoka amtafute Yesu Kristo Mwokozi wao, usiku wa leo; waponye wagonjwa wote na wanaoteseka, Baba, mtumishi Wako anaingia kwa ajili ya huduma, katika Jina la Yesu. Amina!

2 Bwana ambariki kila mmoja wenu. Nina furaha sana kuwa hapa usiku wa leo. Niliingia tu wakati Ndugu Ernie alipokuwa akiimba sehemu ya mwisho ya wimbo wake, Juu ya Mbawa za Hua. Hakika ni shairi zuri, hakika ni zuri, nami na—najua ni la wakati unaofaa. Kwa hiyo sasa, tunashukuru sana.

Na kwa ninyi nyote watu ambao mmesikiliza usiku wa leo kote nchini, laiti mngekuwa tu hapa kuona huku kungoja, matarajio kwenye nyuso za watu wakati wamejaa kwenye jengo hili usiku wa leo; tukiwa na wakati mzuri sana.

Tunataka kumshukuru Ndugu Jack Moore, na Dada Moore, na Ndugu Noel, Ndugu Boutliere, Ndugu Brown, washiriki hawa wote hapa, maskani yote, wafanyakazi wote, kwa kutualika kurudi.

3 Ilikuwa...bila shaka...kama...singesema ni kwa bahati, ilikuwa tu ni mkono wa Mungu uliotenda kazi. Kuna ndugu hapa ambaye aliota ndoto wakati fulani uliopita, kuhusu jambo hili likitukia, alisema mimi "nilikuwa nimesimama nikiwa nimevalia suruali nyeupe, nimevalia viatu vya Kihindi." Na hivyo ndivyo hasa nilikuwa nimesimama nilipomwita Ndugu Jack kwa ajili ya mkutano huu, vivyo hivyo hasa (kule Carson Colorado) viatu vya kihindi na suruali ndefu nyeupe ya aina ya Levi; Ndugu Leo, iwapo unasikiza, nilikuwa nitakutana nawe katika dakika chache tu. Kwa hiyo hapo ndipo mkutano ulipozaliwa, papo hapo.

4 Sasa ni Jumapili usiku; Ninajua wengi wenu mtaendesha magari usiku kucha usiku huu mkienda nyumbani, baadhi yenu mtakuwa mkiendesha gari asubuhi. Nina safari ya siku mbili kwa gari mbele yangu. Na kwa hiyo sisi—sisi hatutawachelewesha sana. Nami nimejaribu kuufanya huu kuwa ni usiku wa kale, usiku ambao Ndugu Brown, na Ndugu Jack, na sisi sote tuliokuwa tukiwaombea wagonjwa miaka mingi iliyopita, tungewaombea wagonjwa kwa njia ile ile tuliyoomba basi.

Sasa, mnaweza kunisikia huko nyuma? Nazidi kuzishusha hizi maikrofoni kwa maana sauti imenipwelea.

5 Na kwa hiyo nataka kuninii ... Kitu kidogo tu, tukio hili dogo limetukia. Naam, wao walikuwa wakiniambia muda mchache uliopita ya kwamba kulikuweco ndugu fulani, huenda yuko hapa mkutanoni usiku huu, ambaye ametoka hivi punde katika udhehebu; akaja kule Shreveport, alitaka kusikia Ujumbe. Naye akachanganyikiwa, hakujua mahali alipokuwa, kwa hiyo akaenda mjini. Aliona watu wamekusanyika, akasema, "Hapa ndipo Billy Branham atakapohubiri?"

Akasema, "La, ni mahali ambapo Billy Graham anahubiri kwa—kwa njia ya—ya sinema."

Akasema, "Vema, samahani, ni—niko mahali pasipofaa."

Yeye alisema alikuja huku, akasema, "Sasa naweza kwenda wapi, Bwana?" Kasema alianza kutembea kwenye barabara hii kuu. Sijui ni kitu gani, kuna kanisa kubwa hapa mwishoni. Mtaa wa Texas. Na kulikuwa na msalaba mkubwa mweupe juu ya kanisa. Kasema Bwana alimwambia, kasema, "'Endelea tu kutembea.'" Kasema ... alipofika kule, kulikuwa na ... Kasema, "Vema, lazima iwe hapa, mna motokaa nyingi sana zimesimama humu." Kisha akasema, "Bibi -arusi na bwana arusi walikuja wakitoka kanisani." Hiyo ilikuwa jana usiku, kulikuwa na arusi, niliona ikitokea. Bwana alisema, "Sasa, hivyo ndivyo ilivyo. Unatoka kwenye udhehebu kuingia katika Bibi -arusi, kwenda pamoja na Bwana Arusi." Mnaona? Mnaona?

6 Nilikuwa nikinena na mke wangu, nilipokuwa nikija barabarani, jinsi mwezi na nyota zilivyokuwa zikining'inia juu ya huo msalaba, tulipokuwa tunaukaribia. Nadhani ninaangalia tu mambo madogo kama hayo, labda kwa namna fulani yanapendeza imani yangu katika Mungu na huduma yangu.

Nilikuwa nikiwaza usiku wa leo, huko Tucson, ilikuwa kwamba Victor Le Doux, yeye alikuwa ni Mfaransa huyu ... yeye ni Mfaransa halisi. Ninaamini nilikuwa nikiwaambia hivi majuzi, ya kwamba nilipomaliza kuzungumza, nikijaribu kutenganisha umadhehebu na Ukristo halisi ... Na mtu fulani alikuwa

akinipa ninii ... namna fulani ya mazungumzo mafupi juu ya jambo hilo, kutoka kwenye kanisa maarufu la Kipentekoste la kimadhehebu.

Na kwa hiyo Danny Henry, nafikiri yeye ni binamu wa staa wa sinema ama cho chote kile, naye alikuwa Mbatisti; naye akakimbilia jukwaani, na kunikumbatia tu na kusema, "Ndugu Branham, natumaini hili halisikiki la kukufuru, lakini hayo yanaweza kuwa ndio sura ya 23 ya Ufunuo." Na wakati alipoanza kusema jambo lingine, alianza kunena kwa lugha.

Na hii, watu watatu wa Kifaransa ... Mwanamke wa Kifaransa (mwanamke mkubwa, mnene, mwenye rangi nyeusi, kutoka Louisiana, huenda akaketi hapa usiku wa leo) aliandika kwenye kipande cha karatasi, yale aliyosema. Ndipo Victor Le Doux, mhudumu, akaandika jambo lile lile; nao walikuwa wakilinganisha maandishi, ama walitaka kufanya hivyo. Mtu mwenye nywele nyepesi (kwa namna fulani nywele za shaba) amesimama huko nyuma kabisa, ameketi kabisa nyuma awezavyo, akaja huku, alitaka kuona maandishi hayo. Alikuwa mkalimani wa Kifaransa katika Umoja wa Mataifa. Na maelezo yote matatu yalikuwa sawa.

Na ilisema hivi:

*Kwa sababu umechagua njia hii iliyo ngumu zaidi ... Umeichagua, umechukua ... uliichagua kwa chaguo lako mwenyewe.*

Bila shaka, tunajua jambo hilo. Ilimbidi Musa kufanya chaguo lake. Kasema:

*Hii ndiyo njia halisi na sahihi, kwa sababu ni NJIA YANGU.*

*Na ni—ni uamuzi mzuri jinsi gani ambao umefanya!*

Kasema:

*Kwa sababu ya jambo hili, sehemu kubwa ya Mbinguni inakungojea.*

*Na hili lenyewe ndilo litakalosababisha, na kutimiliza, ule ushindi mkuu katika Upendo wa Kiungu.*

Zote tatu zilikuwa sawa. Nilifikiri nilikuwa na hilo katika Biblia yangu usiku wa leo, (niliangalia mle ndani, bali sikuliona), nakala yake ya asili.

7 Danny Henry hajui ... kama mimi mwenyewe, ni vigumu kwake kujua Kiingereza kizuri, sembuse Kifaransa. Kama ukiangalia mle ndani, ni kama lugha ya Kifaransa, wanaweka kitenzi mbele ya kielezi. Na tafsiri ya yote matatu ilikuwa sawa kabisa.

Danny Henry, wakati fulani uliopita, alifanya ... Huenda Danny anasikiliza usiku wa leo. Victor Le Doux labda yuko, kwa sababu nafahamu yuko Tucson. Nanyi watu huko Tucson kanisani, maskanini, maskani ya Tucson ambamo Ndugu Green ndiye mchungaji wake; Ndugu Victor La Deaux, nasikia yuko katika mkutano wa hema papo hapo chini ambapo Park Avenue inapoungana na njia kuu ya 80, ikija huku. Na kama uko huko nje kesho usiku na usiku unaofuata, wakati wo wote atakapokuwa kule, nenda ukamsikize; na huenda Danny akawa pamoja naye. Na huenda ikawa kwamba wanasikiliza kutoka kwenye maskani usiku wa leo, sijui.

8 Danny alienda Yerusalemu mara baada ya hayo, na akasema alikuwa amelala pale kwenye kaburi kwenye ubao ... ubao wa mwamba ambao Yesu aliweka, maiti kabla tu ya kufufuka Kwake. Kisha akasema, mara nikaingia moyoni mwake; na akasema alitoka mbio, akaanza kulia, naye akatoka nje. Naye alielekezwa ... Yeye ni mtu anayetengeneza vitu kwa mawe; mawe fulani, namaanisha. Alisema alienda mahali waliposema msalaba ulishushwa chini, naye akaanguka tu ... akagonga kipande kidogo cha mwamba kama ... loo, mraba inchi, ama kitu kama hicho; akakiweka mfukoni mwake, na alivutiwa kukileta nyumbani.

Alipofanya hivyo, kitu fulani kilimwambia, "Mtengenezee Ndugu Branham jozi ya sijafu kutoka kwenye hiyo." Kwa hiyo akakiweka katika ile asidi, nacho kikabadilika rangi kutoka kwenye mwamba wa kawaida wa chokaa ukawa jiwe la rangi ya damu. Naye akatengeneza sijafu.

Naye aliponipa hizo, hakuwa ameona hilo, bali kupitia kwa sijafu hizo mbili mna mstari ulionyoka na mwembamba. Nimezivalia usiku huu, kuwaombea wagonjwa. Mnaona, ka—rangi ya jiwe la jekundu, kama damu inayotiririka; lenye mstari ulionyoka, mwembamba moja kwa moja. Ni vile hasa unabii wake ulivyosema, "njia iliyonyoka na nyembamba"; mnaona, katika unabii. Nilimwonesha hiyo.

Danny, kama unasikiliza, wewe ama Ndugu Le Doux, ye yote yule, usiku wa leo utakuwa usiku wa mtindo wa kale tutakapowaombea wagonjwa. Nina furaha kutembea njia hii iliyonyoka, nyembamba, njia ya Injili, njia ya Neno, pamoja na Bwana wetu Yesu Kristo.

9 Mungu awabariki nyote. Sasa, mnapendeza sana kuzungumza naye, nitazungumza tu kwa muda

mrefu na nitawaweka hapa kwa muda mrefu sana. Billy alisema kuna watu kati ya mia tatu na mia nne watakaombewa, kwa hiyo itanibidi tu kuharakisha na ujumbe wetu upesi iwezekanavyo, kisha niwaombe wagonjwa.

Sasa, kwa watu wa Arizona, Jumamosi ijayo usiku, tuko kule (kamwe hatuwezi kukumbuka jina la mji huo) Yuma, Arizona, kwenye karamu. Kwa hiyo basi, huko California, tunafuatilia moja kwa moja Jumapili asubuhi, kwenda Los Angeles na mahali ambapo imebashiriwa kuwa tutakuwepo.

Usiku wa leo, ninataka kuchukua somo kutoka kwenye Maandiko.

10 Jambo lingine, nilikuwa nimeketi kwenye mkahawa leo, Mkahawa wa Morrison; Ndugu Jack, mkewe, mimi na mke wangu. Tulienda kwenye Cafeteria ya Morrison tupate muda kidogo pamoja, hatukuwa tumetoka, hao wanawake hawajawahi kuwa pamoja kamwe. Kulikuwako na kijana mmoja aliyekuja kwangu, jina lake ni Green, yeye ni baba wa Ndugu Peary Green. Naye akasema, "Unajua, Ndugu Branham, ulikuwa unazungumza juu ya 'pini ya Johnny' usiku uliopita." Hiyo ni kweli ... Ni kitu gani? Ni kibanio kidogo cha chuma. Yeye alisema, "Ulikuwa unazungumza juu ya 'pini ya Johnny,'" kasema, "Nilikutatia 'pini ya Johnny.'" Yeye alinipa mimi.

Sasa, hiyo ni "pini ya Johnny," mabibi, ambayo haitafaa kwa nywele. Pini ya Johnny, yeye alisema— alisema ameitumia kwa miaka kadha, kushikilia kurasa za Biblia yake. Kwa hivyo akasema, "Nitakupa pini ya Johnny" halisi. Kwa hivyo, Ndugu Green, iwapo umu humu mahali fulani ama unasikiza, hiyo ndiyo "pini ya Johnny," iliyo nzuri sana, huzishikilia vizuri.

11 Sasa tunataka kuingia kwenye Maandiko mara moja. Nami nawatakeni mfungue pamoja nami sasa katika Zaburi 55, halafu pia Mathayo 3. Na somo langu usiku wa leo lilikuwa ni mada ya Ndugu Ernie: Juu ya Mbawa za Hua Mweupe. Sasa, sitaweza kugusa maandishi yote na Maandiko niliyo nayo hapa, kwa sababu kwa namna fulani nitaruka baadhi ya hayo, na kwa sababu niliahidi ujumbe.

Bwana akipenda, kwa ajili ya Yuma Jumamosi ijayo usiku, ninataka kuhubiri juu ya: Masharti ya Kanyakuliwa, Bwana akipenda.

12 Katika Zaburi 53 ... samahani, Zaburi 55.

*Sikiza ... (Samahani? 55, naam, bwana.)*

*Ee Mungu; ... uisikilize sala yangu, Wala usijifiche nikuombapo rehema..*

*Unisikilize na kunijibu, Nimetanga-tanga nikilalama na kuugua;*

*Kwa sababu ya sauti ya adui, Kwa sababu ya dhuluma yake yule mwovu. Kwa maana wananiupia uovu, Na kwa ghadhabu wananiudhi.*

*Moyo wangu unaumia ndani yangu, Na hofu za mauti zimeniangukia.*

*Hofu na tetemeko limenijia, Na hofu kubwa imenifunikiza.*

*Nikasema, Ningekuwa na mbawa kama njiwa, Ningerukia mbali na kustarehe.*

*Ningekwenda zangu mbali, Ningetua jangwani. Sela. (Sela maana yake ni "Amina.")*

13 Daudi, mpenda nyika, wakati alipofadhaika na watu wasingemwamini, na maadui walikuwa wamemjia, alisema, "Kama ningalikuwa na mbawa za hua, ningaliruka niende nyikani na imebaki." Ni mara ngapi nimefikiria jambo lile lile! Kama ningeweza kutoa bunduki yangu ukutani, begi langu la kambi, niende nyikani na nisirudi tena. Nimemwomba Bwana kama ninaweza kuishi nione siku ... Sitaki ibada ya mazishi kamwe, nilisema, "Kama ninaweza tu kwenda mwituni mahali fulani, nimwegemeze huyo 'Mweupe' wa kale dhidi ya mti, ..."

Hiyo ni bunduki yangu, samahani, na—na—nasema hivyo kwa sababu ya mke wangu aliyeketi pale. Mwajua, hiyo bunduki, Ndugu fulani hapa alinipa miaka mingi iliyopita, niliwaua wanyama wakubwa hamsini na watano nayo, bila kukosa risasi, baadhi yao wakiwa yadi mia saba hadi mia nane. Ninaiita "Mweupe" kwa sababu mke wangu ana nywele nyeusi, kwa hiyo akasema ninaijali zaidi bunduki kuliko ninavyomjali yeye. Lakini ...

Kwa hiyo, ni—ningetaka kuiegemeza kwenye mti, na kusema, "Bwana, hebu Yusufu akaipate siku moja." Ningependa kuchukua mbawa za hua na kuruka mbali.

Lakini kama tu wakati mmoja kule juu milimani na nilipokuwa namtazama tai, na kumwona akiruka (unajua hadithi yangu), nilisema, "Ni vizuri kuwa hapa, Bwana; kama Petro alivyosema, 'tungejenga vibanda vitatu.' Lakini huko chini kwenye mlima, wagonjwa na wanaoteseka wanangoja, waliopotea na wanaokufa wanangoja." Kwa hiyo hebu na tufanye tuwezavyo wakati kungali mchana, na siku moja kutakuwa na ... mabawa ya Tai mweupe yatashuka, Yeye atatuchukua.

14 Sasa katika Mathayo 3:16, ningetaka kusoma 16 na 17.

*Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake;*

*Na tazama, sauti kutoka mbinguni, ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. (Kwa maneno mengine, "ninayependezwa kukaa ndani yake.")*

15 Sasa tunataka kuzungumza kwa dakika chache juu ya ndege huyu. Njiwa daima amekuwa mmoja wa ndege ninaowapenda sana. Na tukiwaza juu ya hua, hua kwa kweli ... na njiwa ni ndege yule yule. Njiwa ni huwa wa kufugwa. Wote wawili ni familia moja. Nimeiangalia na ni familia ile ile. Njiwa na hua, wote wawili ni wa familia moja. Tabia za ndege hawa ni bora sana.

Nilihubiri hapa, miaka michache iliyopita, katika mkutano wa hema hapa pamoja na Ndugu Moore, juu ya: Mwana -Kondoo Na Hua. Nadhani ninyi nyote mnakumbuka jambo hilo; na jinsi ambavyo hua ndiye ndege aliye msafi sana tuliye naye, na mwana -kondoo ndiye mnyama mpole sana tuliye naye. Wote wawili ni ndege na mnyama wa dhabihu.

16 Namna ilivyoonyeshwa vizuri hapa kwa mfano kwamba Yesu akiwa Mwana -Kondoo, na Mungu akiwa Hua. Na huyo hua asingalitulia juu ya mbwa mwitu, asili yake si sawa. Isingeweza kukaa juu ya mbwa, asili yake si sawa. Ilibidi iwe juu ya mwana -kondoo; tabia hizo mbili zilipaswa kuwa sawa. Na hivyo ndivyo inavyotupasa kuwa, tabia zetu hazina budi kubadilika kutoka kwa mwenye dhambi anayenguruma na kuwa mwana -kondoo mpole.

Na je! Mliona Hua alimwongoza Mwana -Kondoo? Na tazama, Mwana -Kondoo alisalimisha kila kitu alichokuwa nacho kwa Hua. Na angalia mahali ambapo Hua alimwongoza: kusulibishwa kwa ajili ya dhambi zetu sote.

Sasa, Hua wa ... Mungu alitaka kumwakilisha Mwanawe, Yeye aliwakilishwa na mnyama aliye msafi sana na mnyenyekevu kuliko wote duniani, kiumbe cha duniani; bali wakati Mungu alipojiwakilisha Mwenyewe mbinguni, ilikuwa kwa ndege mpole sana na msafi sana aliyeko mbinguni, hua.

17 Sasa, hua hutofautiana, kuna tofauti zao nyingi. Kwa kawaida hua wetu kwa namna fulani ni ndege wa kijivu. Na halafu kuna hua anayeomboleza, na halafu kuna hua wa jioni. Kuna pia anayetwa hua wa sonora tuliye naye nyumbani, yeye ni jamaa mdogo, mwenye mvi; maskini jamaa mdogo mwenye milia miekundu kwenye mbawa zake. Kuna aina nyingi za hua, nao wanatofautiana katika rangi. Kwa hiyo kuna jambo lile lile katika njiwa.

Sasa, hua ni hua aliyeumbwa kwa njia ya kipekee sana, kwa sababu tabia yake ni kwamba hawezi kula cho chote ambacho ni kichafu; hawezi akafanya hivyo kamwe, kwa sababu hakuumbiwa hayo.

18 Sasa, daima nimezungumza juu ya hua kuwa mfano wa Mungu, na kunguru akiwa ni mfano wa mnafiki. Kunguru anaweza kuketi juu ya mzoga wa kale uliokufa na kula, siku nzima, na kuruka moja kwa moja shambani na kula ngano pamoja na hua. Lakini hua anaweza kula ngano vizuri, bali hawezi kula mzoga uliokufa. Mnaona? Hawezi kabisa kufanya hivyo, hawezi kuuvumilia. Nami nilishangaa ni kwa nini asingeweza kufanya hivyo; wote wawili ni jamii ya ndege, wote wawili ni ndege. Lakini kwa nini? Ni maumbile yao.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo halisi. Ninii ... Mkristo wa kimadhehebu tu anaweza tu kuchukua cho chote, bali Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili hawezi kuchukua mambo ya ulimwengu. Yeye ameumbwa tofauti.

19 Niliona ya kwamba hua hana nyongo yo yote. Hakuna nyongo katika hua kwa sababu hana haja nayo.

Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo, yeye hahitaji uchungu wo wote, unaona, maana anaweza tu kula Chakula cha Mungu. Wala haihitaji uchungu kuyeyusha hicho; inahitaji upendo, mnaona, kwa hiyo yeye ... kukiyeyusha chakula. Uchungu: "Loo," wanasema, "vema ..." wanahitilafiana Nalo. Lakini upendo daima hulipokea, Neno la Mungu.

Sasa, yeye hana nyongo, kwa hiyo basi asingeweza ... ni kinyume chake kula cho chote kibaya. Na kama angefanya hivyo, ingemwua. Lakini hakuna hatari yo yote, yeye hatakula (a-ha), kwa sababu hana hamu yake.

20 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo halisi. Je! Ulijua Mkristo halisi hana hata dhambi yo yote iliyohesabiwa kwake? Daudi alisema, "Heri mtu yule ambaye Mungu hatamhesabia dhambi." Unapoosha katika Damu ya Mwana-Kondoo (si kwa kujifanya mwamini, bali kwa kweli ni—ni Damu ya Mwana-Kondoo), Mungu hakuhesabii cho chote kilichofanywa, kwa sababu uko chini ya Damu na Yeye hakioni. Kuna dhabihu ya Damu; kitu pekee anachoweza kukuona ndani yake, ni namna Yeye alivyokuona kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu wakati alipoliweka jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana -

Kondoo. Hilo tu ndilo analoweza kuangalia, kwa sababu umekombolewa kutoka kwa kila kitu kilichopata kufanywa, umeoshwa katika Damu ya Mwana -Kondoo. Kwa hiyo hakuna nyongo ndani yako, hakuna tabia chafu ndani yako, kwa sababu kwamba Damu ya Mwana -Kondoo imefanya hivi; na Mungu hawezi kukuhesabia dhambi baada ya kuwa na sadaka ya dhambi iliyoko pale ikikungojea.

“Vema,” unasema, “hilo linanipa nafasi kubwa basi, Ndugu Branham, ninaweza kufanya kile ninachotaka kufanya.” Mimi daima hufanya hivyo; daima. Lakini wakati mtu anaweza kweli kuona yale Yesu aliyomfanyia, na kugeuka na kufanya jambo fulani kinyume na Yeye, inaonyesha yeye hakumpokea Kristo kamwe.

21 Nina maskini mke wangu anayeketi kule nyuma. Yeye ni mdogo kuliko mimi kwa miaka kumi, na ana mvi kama nilivyo mimi. Sababu yake ni kwamba yeye amesimama kati yangu na—na ulimwengu wa nje. Kama ningenda ng'ambo, nami ninge ... Je, hii si ingekuwa namna ya jamaa inayofaa kuishi nayo, kama ningaliikusanya jamaa yangu kunizunguka nami ningesema: “Tazama hapa, Bi. Branham, inakupasa kufahamu ya kwamba wewe ni Bi. William Branham. Usiwe na waume wengine wakati nitakapondoka. Usimkonyeze mwanaume mwingine macho,” na mambo haya yote. “Msifanye ubembe hata kidogo. Kama ukifanya hivyo, nitakaporudi nitakutaliki.”

Naye angegeuka na kusema, “Sasa, mume wangu mwema, ninataka kukuambia jambo fulani pia. Usimtwe mwanamke mwingine ye yote ukiisha kuondoka. Usifanye *hivi* na *vile*. Kama ukifanya hivyo, jihesabu tu kwamba umetalikiwa ukirudi nyumbani.”

Sasa, hiyo haingekuwa ni familia yenye upendo? Mnaona? La! Kama kweli nampenda ... Ingawa ninaamini kama nilifanya kosa na kuteleza na kufanya jambo fulani baya, ninaamini angenisamehe kwa sababu ananipenda. Na kama angefanya hivyo, ninaamini ningemsamehe kwa jambo hilo; hakika, kwa sababu ninampenda. Lakini kama ninampenda namna hiyo, mradi tu nampenda hivyo yeye hana wasiwasi. Ingawa angenisamehe, nisingemdhuru kwa lolote. Ni—ni—ningejisikia mtu mwenye hatia kuliko wote ulimwenguni, nisingeweza kungojea hata dakika moja ningemwambia kuhusu yale niliyofanya, kwa sababu ninampenda. Vema, hiyo ni ... Kama nampenda kwa upendo wa *phileo* namna hiyo, upendo wangu wa *agape* ungekuwa mkubwa jinsi gani kwa Yesu Kristo?

22 Ingawa huenda nikavuta sigara, sijawahi kamwe maishani mwangu; lakini ingawa ningefanya hivyo, Yeye huenda akanisamehe kwa jambo hilo, ninaamini angefanya hivyo. Kama ningekunywa, sijawi kamwe maishani mwangu, bali ninaamini Yeye angenisamehe kwa hilo. Nami ninampenda kupita kiasi, (Mungu, nisaidie) Sitaki kufanya kitu kama hicho, mnaona, kwa sababu ninampenda. Upuuzi huo huo umeniondokea, kwa sababu Yeye aliponibadilisha kutoka kwa kunguru na kuwa hua kulileta mabadiliko, tamaa ya mambo hayo na kadhalika iliondoka; basi sihesabiwi dhambi kwa sababu sikusudii kufanya hivyo, sina shauku ya kuitenda.

23 Sasa jambo lingine kuu juu ya hua huyu. Yeye ni ndege wa ajabu. Ulipata kuwaona ndege wote ...

Moja ya ndege ninaowapenda sana ni robin. Sasa, ninyi wavulana acheni kupiga risasi robini wangu, mnaona, maana sitaki ninyi mfanye hivyo. Robin wangu, mwajua jinsi alivyopata kifua chake chekundu? Mwajua, siku moja kulikuwako na Mtu akifa msalabani, hakuna mtu angemsaidia, Mungu alikuwa amemwacha Mtu huyo, Naye alikuwa akifa. Mikono Yake ilikuwa na misumari ndani yake, miguu Yake na ubavu Wake ukivuja damu, taji kichwani Mwake na miiba, damu ikitiririka usoni Mwake. Na kulikuwa na ndege mdogo aliyepita, ndege mdogo, wa hudhurungi. Naye akaangalia jambo hilo, alikuwa ... alidhani lilikuwa ni jambo la kusikitisha sana alilopata kuona. Naye alijua alikuwa ni ndege mdogo tu, bali aliitazama ile misumari mikubwa mno mikubwa ya Kirumi iliyopigwa mkononi Mwake, naye akaruka na mdomo wake mdogo na kujaribu kuivuta. Kifua chake chote kikalowa damu, tangu wakati huo kimekuwa chekundu. Ninataka kifua changu kifunikwe na Damu Yake, pia, nikimtetea nitakapokutana Naye. Ninampenda robin mdogo.

24 Lakini, unajua, robini mdogo hana budi kuoga; lakini, unajua, hua haimpasi kufanya hivyo; hapana. Yeye ana aina fulani ya mafuta ndani yake ambayo humpaka mafuta na kumfanya awe safi kutoka ndani hata nje. Mnajua jambo hilo? Yule hua anayo! Njiwa hujipaka mafuta. Je! Uliwahi kuchukua mmoja, kunusa hiyo harufu yake, njiwa ama kitu fulani? Hayo ni mafuta ambayo yanazalishwa kutoka ndani yake. Mwili wake hutengeneza tezi ya mafuta ambayo huweka manyoya yake daima safi nje kwa sababu yeye ni msafi kutoka ndani hata nje. Hiyo ni kweli. Yeye ni ndege mdogo wa ajabu.

Sasa, ninajua mnaweza kuwawinda hapa, nafikiri, huko Louisiana. Usifanye hivyo! Loo, nisingeweza kufanya hivyo. Nadhani ningalikuwa na njaa, ingekuwa sawa, bali si—singalimpiga bunduki ye yote kwa vyo vyote.

25 Kuna ... Hua ana jambo la ajabu sana katika familia yetu. Siku moja wakati bibi yangu ... Alitoka hapa juu Kentucky, kutoka kwenye hifadhi ya Cherokee. Alikuwa anakufa, maskini mwanamke, naye alikuwa ... Walikuwa na ... Nafikiri wanauita ugojwa wa kuvimba matezi ya shingoni au cho chote kile, alikuwa akifa. Naye babu akapiga magoti kando ya kitanda; wakati Mama, Shangazi Birtie, Shangazi Howlie, wote

walipiga magoti kitandani; Mjomba Charlie, (mvulana mdogo, mwenye umri wa miaka minne) mtoto mchanga; Mama, aliye mkubwa kuliko wote, akiwa na umri wa kama miaka kumi na miwili. Naye alikuwa amechanulia nywele zake nyeusi kitandani, naye akaanza kuimba, *"Mwamba wenye imara, kwako nitajificha"*, alipokuwa anakufa. Babu, wakati huo, hakuwa Mkristo. Nilimbatiza akiwa na umri wa miaka themanini na saba, katika Jina la Yesu Kristo, chini ya mto pale ambapo Malaika wa Bwana alitokea.

Lakini wakati alipokuwa akiimba wimbo huu, huku mikono yake midogo imeinuliwa hewani, hua akaruka mlangoni; nikaja, nikaketi juu ya kitanda, nikaanza kulia. Mungu aliichukua nafsi yake.

26 Nilienda huko London, Uingereza pamoja na Ndugu Jack na Ndugu Gordon Lindsay, na kulikuweco mwanamke jina lake Florence Nightingale (anadai kuwa, nafikiri, kitukuu ama cho chote kile cha hayati Florence Nightingale) ambaye aliniandikia barua nyingi. Alikuwa huko Afrika Kusini, akifa kwa kansa. Naye alikuwa na picha; mmeiona katika kitabu. Sijapata kumwona mwanadamu kama huyo maishani mwangu. Ndugu Jack, naamini, alikuwa pamoja nami siku hiyo. Tulienda kwenye nyumba ya mhudumu, nyumba ya kasisi, nyuma tu ya kanisa ambako walikuwa wamemleta.

Tulipokuwa tungali huko nje kwenye ... mahali ndege iliposhuka, wakaita majina yetu, naye alikuwa kwenye gari la wagonjwa pale wakati huo; nilikuwa nimepelekwa kwa ndege kutoka—kutoka huko Afrika Kusini, nikijua ya kwamba nilikuwa nikija Uingereza wakati huo. Mhudumu alimpeleka kwenye nyumba ya kasisi, kwa hiyo tukarudi kule kumwomba.

27 Nimewaona watu wengi sana walio wagonjwa, lakini mikono yake midogo haikuonekana yenye upana unaozidi inchi moja, fu—fuvu lake la kichwa mahali lilipounganishwa, ungeweza kupaona. Naye...viungo vyake humu juu kabisa karibu na kiuno chake havikupita hivi, yapata inchi mbili kutoka upande mmoja hata mwingine, mfupa tu. Naye hangeweza kuinua mikono yake, alikuwa mnyonge sana kuinua mikono yake. Naye alikuwa akijaribu kusema jambo fulani, nami sikuweza kumsikia. Na wakati hatimaye niliposikia, ninaamini kupitia kwa nesi, alisema, "Ndugu Branham, omba ya kwamba Mungu ataniacha nife." Hangeweza ... hakutaka kuishi. Nami nikaona, na machozi yalikuwa yakitiririka upande wa huo mfupa usoni mwake. Alikopata unyevu wa kutosha ndani yake kulia, sijui mimi; kwa maana mishipa yake ilikuwa imebonyea, naye alikuwa katika bali mbaya sana. Kwa kuwa nilikuwa nimekuja kuwaomba wagonjwa, nisingeweza kumwomba afe. Lakini alionekana tu kama asingeweza kufa, aliendelea tu kuishi.

Nikapiga magoti pamoja na mchungaji wenu, chumbani kuomba. Na wakati nilipopiga magoti kuomba, hua mdogo akaruka dirishani; akaanza kulia kwa sauti nyororo. Nilipomaliza kuomba, nilifikiri ilikuwa ni hua aliyefugwa pale mahali fulani. Kulikuwa na ukungu nje, jinsi Uingereza ilivyo, Visiwa vya Uingereza kule. Ndipo maskini hua huyu akaacha kulia, akaruka akaenda zake. Nikaenda pale nikamwekea mikono na kuliita Jina la Bwana. Na yule mwanamke ni bibi mkubwa mno na mwenye nguvu na afya siku hizi juu ya mbawa za Hua.

Yeye hujiweka safi kutoka ndani. Mkristo akifanya hivyo pia, yeye husafisha kutoka ndani. Hilo huondoa uovu ... Yeye hahitaji nyongo yo yote kumeng'anya cho chote, kwa sababu yeye huwa hali kitu hicho. Mnaona? Yeye ni msafi tangu ndani hata nje.

28 Sasa, tunaona ya kwamba ndege huyu ... Mambo mengi nimeyaandika hapa chini, lakini saa inaendelea kuzunguka. Ndege huyu pia alitumiwa katika Agano la Kale kwa ajili ya dhabihu, kwa ajili ya upatanisho na kwa ajili ya utakaso. Hebu turejee hapa moja kwa moja katika Mwanzo 15:9. Hebu na tufikirie kifungu hiki kwa muda kidogo tu. Sasa, Ibrahimu alikuwa ... alimwuliza Mungu hapa, angefanyaje jambo hili. Na Mungu analirudisha Neno Lake kwa Ibrahimu, Naye analifanya kwa njia ya ajabu. Tuanzie karibu na ... Hebu tuanze kwenye kifungu cha kwanza. Msipende kuharakisha jambo hili.

*Baada ya mambo hayo neno la Bwana likamjia Abramam katika njozi, ...*

Mnaona, Ibrahimu alikuwa ni nabii, kwa hiyo aliona maono.

*... Usiogope, Ibrahimu; Mimi ni ngao yako, na ... dhawabu yako kubwa sana. (Yehova-Manesses, unaona.)*

*Ibrahimu akasema, Ee- ... akasema, Bwana MUNGU ... (Angalia, herufi kubwa L, "Bwana MUNGU." Elohimu! Unaona?) ... Bwana MUNGU, ... (katika njozi) ... utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto, na atakayeiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri, Mdameski?*

*Abramu akasema, Tazama, hukunipa uzao, na mtu aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu.*

*Neno la BWANA likamjia, kusema, Huyu hatakurithi; ...*

Nimempa ahadi, mwajua. Si ... Mnaona, papo hapo Ibrahimu angeshindwa, bali ahadi hiyo haina masharti; lile agano, lisilo na masharti.

*... bali atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayekurithi. (Naye ana umri wa miaka mia*

moja sasa.)

*Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. (Mtu asiye na mtoto, na sasa ana umri wa miaka mia moja.)*

*Akamwamini Bwana, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.*

*Kisha akamwambia, Mimi ni Bwana, niliyekuleta kutoka Uru wa Wakaldayo nikupe nchi hii ili uirithi.*

*Akasema, Ee- ... Bwana Mungu... ama Bwana, nipateje kujua ya kwamba nitairithi?*

Sasa sikilizeni jambo hili.

*Akamwambia, Unipatie ndama wa miaka mitatu, na mbuzi mke wa miaka mitatu, ... (angalia hao watatu sasa, "umri wa miaka mitatu") ... na kondoo mume wa miaka mitatu, na hua, na mwana njiwa. (Wote wawili ni watu wale wale, wote ni kitu kile kile. Unaona, ilitumiwa katika dhabihu kwamba alikuwa akimwonyesha Yesu mbele.)*

29 Agano lilifanywa ... Mnajua, jinsi alivyowagawanya, na jinsi ambavyo hii ...

Ama nyakati za kale, walipochukua ... walifanya agano, wangechukua na kuandika ma—mapatano. Na kumwua mnyama, kusimama katikati yake; kurarua agano vipande viwili, mtu mmoja alichukua sehemu moja ...

Kama vile dobi wa Kichina alivyokuwa akifanya. Yule Mchina hapa, asingeweza kuandika Kiingereza, kwa hiyo aliandika pale na kurarua kipande cha karatasi na kukupa sehemu. Nanyi—ninyi mnakumbuka madobi wa Kichina walipokuwa wakifanya hivyo. Nawe...sehemu hizo zao mbili ilizibidi kulingania, kusudi upate nguo zako. Mnaona, usingeweza kumdanganya, maana alikuwa na ile sehemu nyingine. Ungeweza kuandika jina lako, bali haungalipasua hiyo karatasi tena ikalingane. Mnaona? Kwa hiyo, yeye alikuwa ... ilibidi iwe ni karatasi ile ile.

Kwa hivyo hivyo ndivyo walivyofanya katika zamani za Kimashariki, zamani...ama zamani za kale katika siku za Kimashariki. Wangemuua mnyama, wasimame katikati yake, wararue kipande cha ngozi ya mbuzi, mmoja akachukua kimoja ... Na wakati agano lilipothibitishwa, walileta vipande pamoja na ilibidi viumane kabisa.

30 Sasa, kile Mungu anachomwonyesha hapa ni hiki, juu ya dhabihu hizi, zinanena juu ya Kristo; ya kwamba namna Mungu alivyompeleka Yesu Kalvari na kumrarua, na kuupokea huo mwili juu Mbinguni na kumtuma Roho juu yetu, ya kwamba Roho yule yule aliyekuwa juu Yake hana budi kuwa juu yako upate kuungana na huo Mwili, uwe Bibi -arusi. katika wakati wa mwisho. Mnaona? Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Haitakuwa dhehebu, sasa. Itakuwa ni Neno, kile alichokuwa. Mnaona?

Lakini kama vile Neno hilo halina budi kuja kwenye Neno, kama seli ndani ya mwanadamu. Unajua, wakati mwili wa—wako unapojengwa, si seli moja ya mwanadamu, ya pili ya mbwa, na ya pili ya nguruwe. Loo, la, la. Wote ni seli ya mwanadamu. Hivyo ndivyo Mwili wa Kristo ulivyo, Neno wote la Mungu. Si sehemu Yake tu, mapokeo fulani yaliongezwa Kwake; la, wote ni Mwili wa Kristo.

Sasa, tunaona hapa ya kwamba alitumia hua na njiwa, kwa sababu wao ni familia ile ile. Sasa, mara nyingi mna ...

31 Kwa hiyo angalia (ninataja tu Maandiko haya machache) Mambo ya Walawi 12, na aya ya 6. Tunaona hapa ya kwamba utaratibu wa mwanamke kutakaswa; kama mwanamke huyo alikuwa na mtoto mchanga, ilimbidi kungojea. Kama ilikuwa ni mvulana, ilimbidi kungojea kwa muda wa siku thelathini na tatu kabla hajaingia katika kusanyiko pamoja na hua, kwa ajili ya utakaso. Kama alikuwa na msichana, ilimbidi kungojea siku tisini na sita kabla hajaingia katika kusanyiko.

Sasa tunaona hapa, aya ya 6.

*Kisha hizo siku za kutakaswa kwake zitakapotimia, kwa ajili ya mwana, au kwa ajili ya binti, ataleta mwana-kondoo wa mwaka mmoja kuwa sadaka ya kuteketezwa na kindi la njiwa, au hua, kuwa sadaka ya dhambi, awaleta mlangoni pa hema ya kukutania, na kumpa kuhani:*

Mnaona, yeye hawezi kuingia bado kwa sababu siku zake hazijakwisha bado, bali anaweza kumpa huyu ku—kuhani mlangoni, kwa ajili ya sadaka yake. Mnaona, aidha hua ama njiwa mdogo. Wote wawili ni familia moja.

32 Sasa ili—sasa ilitumiwa kwa upatanisho, na katika upatanisho kwa ajili ya dhambi, hua mmoja. Ama kwa ukoma ambao ni mfano wa dhambi ulileta hua wawili: kichwa cha mmoja kilikatwa, akainamishwa juu

chini na kunyunyiziwa huyo mwingine; kisha huyo mwingine akaachiliwa huru. Na wakati hua aliporuka, aliosha ardhi kwa damu ya mwenziwe, na damu ikamlilia Mungu, "Mtakatifu! Mtakatifu! Mtakatifu ni Bwana Mungu!"

Hivi hamwezi kumwona Mwenzi anayekufa, Yesu Kristo? Aliuawa na kunyunyiziwa juu yetu, ili kwamba tuwe huru, tukipaza sauti "Mtakatifu! Mtakatifu! Mtakatifu! kwa Bwana." Ni mifano mizuri namna gani. Laiti ningalikuwa na sauti.

33 Sasa mfano wa Roho Mtakatifu mkuu kama tulivyosoma katika Ufunuo 3:16; alitumiwa na Mungu kwa ishara, huyu hua.

Nuhu alipewa ishara, kama yule ndugu alivyokuwa akiimba juu yake. Mungu alichukizwa, wala hakukuwa na kitu cho chote kinachoweza kuzuia hasira Yake, kwa maana Yeye alisema, "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa." Naye Nuhu alikuwa amepata neema kwa Mungu na alikuwa amejenga safina kulingana na ujenzi ... maagizo, hasa, ambayo Yeye alikuwa amempa. Naye alikuwa ameelea juu.

Naweza kuwaza...yaliyotendeka siku hizo wao waliposema, "Mzee huyu kule juu kilimani, mzee mlokole, akijenga safina, akisema, 'itanyesha', na haijanyesha kamwe." Lakini ni ...

Nuhu alisema, "Itanyesha, hata hivyo."

Na halafu ninajua siku aliyoingia, nafikiri ninii ... siwezi kufikiria ilikuwa ni siku gani, naamini tarehe kumi na saba ya Mei. Nuhu aliingia ndani ya safina, na Mungu akafunga mlango.

Na mawingu yakaanza kuja, mvua zikaanza kunyesha, mifereji ya maji machafu ikaanza kujaa, chemchemi za kilindi zikafunguka, visima vyote vikatiririsha maji yake. Hatimaye watu waliingia majumbani, wakapanda juu. Lile sanduku la kale lilika papo hapo vivyo hivyo.

Muda si muda wakati maji ya kutosha yaliizunguka, ikaanza kuinuliwa juu zaidi na zaidi. Watu walibisha milangoni na kupiga makelele, lakini haikufaa—haikufaa kitu, Nuhu asingeweza kuufungua mlango. Mungu aliufunga, Mungu Ndiye pekee anayeweza kuufungua.

Ndivyo ilivyo kwenye Sanduku letu, Yesu Kristo; Mungu alitufungulia mlango pale Kalvari, Yeye ataufunga hakika tu kama alivyoufungua.

34 Nayo ikaelea, zaidi na zaidi, huenda ikawa kina cha maili moja juu ya uso wa dunia wakati dunia hii ilikuwa ikitapatapa kutoka kwa...kutoka kwa mzunguko wake wa kawaida. Na ikazunguka na kuzunguka, na vipande, na miti, na juu ya milima na kadhalika, ikienda mrama kwa siku arobaini mchana na usiku.

Na pepo zitakapoanza kutulia ...

Hasira ya Mungu ni mbaya sana. Upendo Wake ni safi na wa Kiungu; na hasira Yake ni ya Kiungu—ni ya Kiungu tu kama upendo Wake ulivyo, kwa sababu, Yeye hana budi kutoa hukumu kwa sababu Yeye ni hakimu. Yeye ni mtoa sheria, na sheria isiyo na adhabu si sheria. Kwa hiyo lazima kuwe na adhabu kwa sheria. Nawe unakiuka sheria za Mungu, hapo ndipo unapolipa adhabu.

35 Sasa tunaona ya kwamba baada ya Nuhu kuelea kule juu, bila shaka aliugua ugonjwa wa bahari kwa sababu ya kunguruma huko kote na vishindo, na hasira ya Mungu ikipondaponda na kusaga, na mayowe na kadhalika. Ndipo ikaanza kutulia, hakuna kilichotukia. Siku zikapita, hakuna kitu kilichotukia. Labda chakula cha wanyama na kadhalika kilipungua, hakuna kitu kilichotukia. Kwa hiyo akawaza, "Nashangaa ... Siwezi kuona nje."

Safina ilijengwa hivi kwamba (mara ulipoingia ndani), kulikuweco dirisha moja tu ndani yake, nalo lilikuwa juu kabisa. Usingeweza kuangalia upande, usingeweza kuangalia njia nyingine ila moja kwa moja juu. Na hivyo ndivyo Sanduku, Yesu Kristo lilivyo. Huwezi kumtazama jamaa mwingine, huwezi kuangalia kitu cho chote ila Kristo ukiwa ndani ya Safina kwa sababu kuna mlango mmoja tu, Naye Ndiye ule Mlango tuliozungumza habari zake asubuhi ya leo. Inakupasa uzidi kutazama juu, "Kwa sababu atakayetia mkono wake kulima, kisha akageuka akaangalia nyuma, hafai kwa kulima."

36 Sasa, kama katika safina hii ... Naye angeweza kuona nuru, na labda nuru ya jua, bali alishangaa alikuwa wapi. Safina ilikuwa ingali inaelea, angeweza kusikia mawimbi yakipiga pande zake safina, lakini alijua siku nyingi zilishapita, hakika maji yalikuwa yamepungua kufikia wakati huo. Kwa hiyo akaenda na akamchukua ndege asiyeaminika, mwenye hila, naye akamjaribu, naye akamtuma. Yeye alikuwa kunguru, na huyo kunguru hakurudi kamwe, kwa sababu alipata anasa huko nje, nje ya sanduku la Mungu. Aliruka toka kwa mzoga mmoja hata mwingine, akila mizoga na nyama zilizooza ambazo zilielea majini; naye aliridhika kabisa.

37 Kwa hiyo baada ya siku kadhaa alijaribu tena, kwa kuwa alijua ... Hakutaka kutoka nje kwenye hasira ya Mungu. Kwa hiyo akamwachilia hua. Na hua huyu alikuwa wa tabia tofauti na ... Hakuwa mwewe, wala anayekula vilivyoza, yeye hula tu vitu visafina halisi. Naye alikuwa ameridhika kabisa kwa sababu



hangepata cho chote cha kuwekelea nyayo za miguu yake, akarudi safinani. Nuhu akasema, "Vema, mafuriko yangali yanaendelea."

Ndipo akangojea siku zingine kadhaa, naye akatuma tena; kama vile maombi yake, "Ee Mungu, je! hasira Yako imetulizwa? Je! Ghadhabu Yako imekwisha, Bwana? Je, yote yamekwisha?" Naye akasema, "Sasa, kama nikimtuma wakati huu, huenda akaishi huko nje kama mafuriko yamepungua, anaweza kukaa." Lakini yeye alimtuma nje kwa maombi, na ndipo wakati alipotoka akaenda kule kwa kuongozwa na Mungu, akachukua jani la mzeituni kutoka kwenye mti, na akaruka akarudi na kudonoa dirishani tena.

Mungu alitumia hua kama ishara. Akarudi akisema ya kwamba "gharika imekwisha," ndipo Mungu akaufungua mlango, nao wakatoka. Hiyo ni Mwanzo 8:8.

38 Pia limetumika katika Mathayo 3:16, tena wakati hasira ya Mungu ilipokuwa duniani. Wala hakukuwa na njia, usiku wenye giza sana, usiku wa manane, makanisa yalikuwa yamepotosha mambo sana hata hakukuwa na njia ya kuyaepuka. Na kulikuwako na waalimu wa uongo, kila namna ya mambo yakijitokeza, kila aina ya taaluma zikitokea, bali Mungu alimtumia hua tena. Ilimpendeza, Mwanawe Yesu alikuwa amempendelea Yeye sana, hata akamtambulisha.

Sasa, wao hawangaliamini ya kwamba huyu mtoto mchanga aliyezaliwa mle zizini katika hori la majani makavu...kabla baba yake na mama yake, walivyodhaniwa kuwa, hawajaona. Wasingeweza kuwazia Mungu akitumia kitu kama hicho. Kwa hiyo ilimbidi kutambulishwa kwa ulimwengu; na siku hiyo kule chini mtoni, wakati aliposhuka kwenda kujithibitisha Mwenyewe kuwa Kipeo cha Mungu (ambacho nilinena habari zake asubuhi ya leo) ... Alipokuwa mtiifu kuingia majini ...

39 Sasa, kama ukiangalia pale, kuna somo kuu. Yohana alikuwa ndiye mtu mkuu kuliko wote duniani, wakati huo. Yesu alisema, "Hakuna mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama yeye," kufikia wakati huo. Naye alikuwa ni nabii. Unaamini jambo hilo? Sasa, kumbukeni, kama Neno la Mungu litakuja kwa cho chote nchini, itakuwa ni nabii. Hiyo daima ni njia ya Mungu. Je! Unaamini ya kwamba Yesu alikuwa Neno lililodhihirishwa katika mwili? Kwa hiyo kuna njia moja tu anayoweza kuja kutambulishwa; si kwa makuhani.

Yeye hakupanda juu na kusema, "Kayafa, utanitambulisha?" Kama alifanya hivyo, Yeye alifanya kosa lile lile alilofanya Daudi katika somo letu hivi majuzi; mnaona, kama Yeye alienda kanisani, na kusema, "Je! utanitambulisha?"

40 Angalia tu wakati alipozaliwa, hata hivyo. Wakati alipozaliwa, alizaliwa katika kivuli cha kanisa. Na labda walikuwa wakipiga kengele na kila kitu, bali ni wachungaji waliomtambua, na Mamajusi. Mnaona?

Naye yupo hapa sasa, kwenye ... tayari kwa ajili ya huduma Yake. Na kama Yeye ni Neno ...

Kulingana na mpango mkuu wa Mungu, Neno linaweza tu ... "Bwana Mungu hatendi neno lo lote mpaka atakapolifunua kwanza kwa watumishi Wake manabii." Huo daima ni mfano Wake, hauna budi kuwa; wakati ile Mihuri ilipofunguliwa, wakati wowote ule mwingine. Tukio lolote kuu linalotendeka duniani, Mungu hulifunua kwa manabii Wake.

Naye Yohana alikuwa nabii, kwa kuwa alikuwa akitabiri "Yeye angekuja."

Kisha kule chini kandoni mwa kilima siku moja...wakati mahojiano yalikuwa yakiendelea, kundi la makuhani wakisisimama huko. Nao wakasema, "Unataka kuniambia ya kwamba unajiita 'nabii,' na kusimama pale kwenye matope hayo?" (siyo katika kanisa, kwa sababu wasingemkubali) "Simama juu ya matope hayo, na uniambie ya kwamba saa inakuja ambapo Yehova mkuu aliyeamuru sadaka hizi, wakati Yehova mkuu aliyejenga hekalu hili, ambaye aliingia humo kama Nguzo ya Moto, 'siku itakuja ambapo hiyo sadaka ya kuteketezwa kila siku itaondolewa?'"

Yeye alisema, "Atakuja Mtu, Naye yuko miongoni mwenu sasa (mahali fulani huko nje), Naye ataondoa dhambi." Kasisi huyo alikuwa akijadiliana naye.

41 Yohana akaangalia juu! Sasa, yeye ni nini? Nabii! Na hili hapa Neno, hapo linakuja Neno likija moja kwa moja kwa nabii, moja kwa moja majini. Yohana alisema, "Tazama, Mwana -Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Huyu hapo, huyo ni Yeye." Yesu kamwe hakunena neno, akatoka akaenda moja kwa moja majini. Nami ninaweza kuona pale, wamesimama kwenye maji hayo (wazia juu ya mchezo wa kuigiza), watu wawili walio wakuu sana waliowahia kuja duniani: Mungu Neno, na nabii Wake.

Angalia, Neno limekwisha kuja kwa nabii katika kipindi hiki cha neema, majini (a-ha). Nilifikiri mngelipata hilo (a-ha). Katika maji! Ufunuo wa kwanza wa Neno ulikuwa majini. Sasa mnaona ambapo Bibi-arusi alianza, Ujumbe wa nuru ya jioni? Katika maji! Neno, Neno la kweli halijachanganywa na kanuni za imani, bali lilimjia nabii majini, kwa maji.

42 Angalia! Ungeweza kuwazia macho ya Neno na macho ya nabii yakikutana majini? Loo, hilo linanizidi sana. Huyu hapo amesimama nabii, huyo hapo amesimama Neno, wakitazamana machoni mwao. Naye

nabii akasema, "Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe, mbona waja kwangu?"

Nalo Neno lilisema ... Haina budi kuwa ni kweli.

Sasa hebu nitoe mchezo wa kuigiza hapa:

"Yohana, wewe ni nabii, unajua Neno." Mnaona? "Unanitambua, unajua Mimi ni Nani."

"Ninahitaji kubatizwa na Wewe," Yohana alisema.

Yesu alisema, "Kubali iwe hivyo. Hiyo ni kweli kabisa, wewe unahitaji kubatizwa na Mimi. Lakini kumbuka, Yohana, ukiwa nabii, ndivyo itupasavyo, au ni wajibu wetu (kama Neno na nabii), kutimiza kila Neno (a—haa). A-ha. Kwa kuwa, Yohana,"(huu hapa ufunuo sasa)"Yohana, unajua Mimi ni Nani, Mimi Ndimi ile Sadaka. Na kulingana na Neno la Mungu, sadaka ilibidi ioshwe kabla haijatolewa kwa ajili ya sadaka." Hiyo ni kweli? Neno ... "Mwana -kondoo alioshwa kisha akatolewa kwa ajili ya sadaka, nami ni yule Mwana -Kondoo. Nami sina budi kuoshwa kabla sijaweza kutolewa kwa ulimwengu kwa ajili ya dhabihu. Kubali iwe hivyo, Yohana, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kama Neno na nabii pamoja."

43 Vema, hakuwezi kuwa na kosa. Sasa, kila moja ya mambo haya ...

Sasa, mnaona, kama haungekuwa utaratibu huo, Yohana angekuwa kama wengine wetu; kwa hiyo wanasema, "Naam, na—najua Wewe ni nani, Bwana."

"Vema," Yeye akasema, "ngoja kidogo, mimi ni Neno. A-ha. 'Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno.' Hawa aliacha a-ha, lakini huna budi kuchukua kila Neno. Nami ni Dhabihu hiyo, na sina budi kuoshwa kabla sijatolewa. Lakini uliyosema, Yohana, ni kweli."

Yohana akiwa ni nabii, akijua Neno lilipaswa kutimizwa, alilivumilia hilo na kumbatiza. Na wakati alipofufuliwa kutoka majini, ukaja Ujumbe kutoka Mbinguni juu ya mbawa za Hua, "Huyu ni Mwanangu mpendwa." Yeye alituma Ujumbe wa ukombozi wa neema juu ya mbawa za Hua, akaja akiruka kutoka mbinguni. "Duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." Sadaka ilikuwa tayari papo hapo; alikuwa amekuzwa, akalishwa, huduma Yake ilikuwa tayari, Neno ambalo lingeukomboza ulimwengu mzima, "Imekwisha?"

44 Hua hutumika katika Biblia kama mfano wa amani, na pia inatumiwa na mataifa kama mfano wa amani. Tuna mataifa ... Taifa letu linawakilishwa na tai. Na kuna ndege wengine wa mataifa mengine, Rumi ina tai, Ujerumani ina tai; wengi wao, ndege wakuu wa angani. Lakini katika yote, hua anaonyesha amani katika mataifa yote. Ni jambo la ulimwengu mzima.

Kama tu vile Ndugu Green alivyosema usiku mmoja, Ndugu Peary Green alisema, "Ishara ya kujisalimisha ni 'kuinua mikono yako.' Taifa lolote, kuinua mikono yako, ni kujisalimisha." Yeye alisema, "Mnapoimba, mkiinuai mikono yenu, mnasalimisha yote."

Na hua ni mfano wa amani katika kila taifa. Kwa nini amefanywa kuwa hivyo? Kwa sababu ya upole wake, na kwa sababu ya kutokuwa na hatia. Hiyo ndiyo sababu yeye ni mfano wa amani.

45 Jambo lingine kuhusu hua, ni ndege anayependa nyumbani. Anapenda kukaa nyumbani.

Na jambo lingine ni kwamba, daima ni mwaminifu kwa mwenzi wake. Hua, wa kiume ama wa kike, hawaachani. Huyu wa kike humwona mwenzi wake katika majira ya kupandana. Mnaona, hiyo ni sifa kwa uumbaji mkuu wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu alimfanya Hawa kuwa kitu kilichotokana na kingine. Mnaona? Kama angaliumbwa kama jike wengine, wakati wake ulipofika wa kupata mimba, angalimpata mwenziwe; bali angefanya hivyo wakati wo wote. Mnaona? Na hivyo ndivyo ilivyo, hivyo ndivyo ilivyo. Nina ninii tu ... Hatutaki kuingia katika jambo hilo, kwa sababu ninalo juu ya *Ndoa Na Talaka*, na kadhalika. Na namna gani ... Lakini hata hivyo yeye ni mheshimiwa na alileta nguvu hizo, nanyi mnajua jinsi nilivyohubiri habari zake hivi majuzi usiku. Vema, angalia, yeye ana jukumu kubwa.

Lakini hua daima ni mwaminifu kwa mwenzi wake. Daima! Kamwe hamwachi.

46 Na hebu nisimame hapa kwa muda kidogo tu, kusema jambo hili: Bibi -arusi wa kweli, hua wa kike, ni mwaminifu kwa Mwenzi wake, pia. Haitaingiza mafundisho yo yote ya sharti, mafundisho yo yote ya kimadhehebu, chochote cha ulimwengu. Atadumu mwaminifu kwa Mwenziwe, Neno; daima mwaminifu.

Na kwa mwenendo huu wa kupenda nyumbani, kwa matendo yake ya upendo wa nyumbani, ametumiwa kwa ufanisi kama njiwa mbebaji. Kwa sababu anapenda nyumbani, ukimwachilia mahali popote, daima atarudi nyumbani. Atarudi nyumbani.

Tungependa kuisitiza jambo hilo kwa kitambo kidogo, nanyi Wakristo mngefahamu ninachomaanisha. Kila mara atarudi nyumbani, kwa hivyo basi ametumiwa kama njiwa mbebaji. Anatumiwa wakati wa vita, ilikuwa hivyo; wangali wanawatumia, njiwa wabebaji kubeba ujumbe. Kwa hiyo mnaona basi, hilo linamfanya hua, kwa Mungu na mwanadamu pia, mjumbe; hua ni mjumbe. Alikuwa ni mjumbe kwa Nuhu,

kumwambia Nuhu ya kwamba “kuna amani tena.” Alitumiwa na Mungu kuthibitisha ya kwamba huyu alikuwa ni Mwanawe, “Sadaka ya kuleta amani juu ya nchi na nia njema kwa watu.” Alitumiwa kama mjumbe.

47 Papa hapa nina hadithi ndogo moyoni mwangu, nilisoma kitabu kimoja wakati mmoja. Sasa, sitaki kusema jambo hili ni hakika, huenda ikawa katika *Mwisho wa Vita vya Kwanza vya Dunia*. Sina hakika ya hilo sasa; mkikosa kuiona basi nimekosea. Mimi ama nilisoma katika kitabu fulani ... imekuwa miaka mingi iliyopita. Bali bila shaka ilikuwa ni—ni...kusema kweli ni—ni jambo la ajabu lililotendeka.

Askari wa Kiamerika walikuwa wamenaswa na mashambulizi ya bunduki za rashasha za Kijerumani, nao walikuwa katika kitu kama shimo. Ninyi askari, nadhani, mnaelewa jinsi walivyokuwa kwenye upelelezi mahali fulani. Nao wakanaswa, nao walikuwa tu na risasi chache tu zilizobakia. Na Wajerumani walikuwa wakisonga mbele katika vikosi vikubwa, wakija kutoka kila mahali. Nao walijua ya kwamba isipokuwa wangepata kuimarishwa, msaada fulani, ya kwamba hivi punde wote wangekufa; (iliwabidi) Wajerumani wakishuka moja kwa moja kutoka mlimani, wakiangalia moja kwa moja shingoni mwao, wakiingia moja kwa moja ndani yao namna hiyo.

48 Na mmoja wao akakumbuka ya kwamba alikuwa na hirizi ndogo, njiwa mdogo. Kwa hivyo alijua ya kwamba huyu njiwa, kama angalitoka pale, angalipeleka ujumbe kwa makao makuu ya hicho kituo chao. Na kwa hivyo wao wakaketi chini na kuandika kijibarua, “Tumenaswa mahali fulani katika sehemu fulani. Tumeishiwa na risasi, katika masaa machache itatubidi kujisalimisha, la sivyo, tutauawa ovyo ovyo.” Nao walibandika jambo hili, ama walilifunga kwenye—kwenye mguu wa hua huyu mdogo na kumwachilia.

Sasa, yeye ni ndege anayependa nyumbani, kwa hiyo yeye ... anafanya nini? Anarudi nyumbani kwa ajili ya ... kukutana, kumtafuta mwenzi wake. Alikuwa na wasiwasi juu yake, itambidi kurudi nyumbani.

49 Na alipokuwa akipanda kwenda juu, Wajerumani waliona kilichokuwa kimetukia. Kwa hiyo jambo walilofanya, walianza kumpiga risasi yule hua. Na mmoja wao akampiga kwa bunduki ya rashasha kipimo cha .30 au risasi, ikavunja mguu wake. Nyingine ikapasua kipande kikumbwa mgongoni mwake. Kifua chake kilichubuliwa kutoka upande hadi mwingine. Moja ya mbawa zake ikavunjwa, ncha yake ikavunjiliwa mbali, naye akaruka kwa upande. Lakini aliendelea kupanda, na hatimaye akafanikiwa. Huku amelemazwa; akajeruhiwa, akavunjwa, akachubuliwa, bali alianguka mle kambini akiwa na ule ujumbe. Huyo alikuwa ni hua mkuu.

Ila, lo, ndugu, Isaya 53 inatuambia juu ya Mmoja, kashuka kutoka Nyumbani akiwa na yote yaliyokuwa mema:

*Naye alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; na kwa kupigwa kwake sisi tuliponywa.*

50 Magonjwa, ushirikina, na mashetani yalikuwa yametunasa, hakukuwa njia ya kuepukia, kanisa lilikuwa limekosea, walikuwa wameenda kombo kwa mambo ya kidhehebu (na Mafarisayo, Masadukayo, na kutakaswa kwa vyungu na sufuria), na Neno la Mungu likatanguka. Lakini huyu Hua mdogo alishuka, na kuna jambo moja tu lingeweza kutukia: ilibidi kuwe na mkombozi.

Lakini akiwa amejeruhiwa, amevunjwa, amepigwa, ameraruliwa, bali alijua njia Yake ya kurudi Nyumbani. Kwa hivyo kutoka kwenye msalaba wa kalvari walikomchubulia, wakamponda-ponda, wakamrarua-rarua kama kundi la mbwa-mwitu juu yake, yeye aliruka kutoka kalvari na kutua kwenye milango ya Mbinguni, akisema, “Imekwisha! Imekwisha! Wao wako ni huru! Magonjwa yanaweza kuponywa sasa! Wenye dhambi wanaweza kuokolewa! Waliofungwa wanaweza kuwekwa huru!”

Ingawa Yeye alikuwa amechubuliwa na kujeruhiwa, ile vita kuu pale wakati hata kila kitu kilikuwa dhidi Yake ... Hata mshairi alipaza sauti:

Huku miamba ikipasuka na mbingu zikitiwa giza,  
Mwokozi wangu aliinamisha kichwa Chake na kufa;  
Bali pazia lililofunguka lilifunua njia  
Kuelekea furaha za mbinguni na siku isiyo na mwisho.

51 Nimekuwa na ugojwa wa neva maishani mwangu mwote. Nilipokuwa mvulana mdogo kuna kitu kilichonitokea, ambacho kilinitisha, yapata kila miaka saba kingetokea kwangu. Ndugu Jack anakumbuka nilipoanza kwa mara ya kwanza, nilitoka uwanjani kwa mwaka mmoja; jambo fulani lilitukia.

Ninakumbuka siku ambayo Juanita Hemphill ... Nafikiri jina lake ni Juanita Kelly sasa, aliolewa na Ndugu Kelly baada ya kifo cha mumewe. Anna Jeanne, nina picha zao na kadhalika, walikuwa ... Naye ... Na hao wasichana wawili na Dada Moore walikuwa wa—wa watatu. Waliimba wimbo huo ambao kamwe siusahau: *Kuangalia Ng'ambo ya Machweo*. Ndugu Jack, unakumbuka, nadhani, nikija kutoka Florida. Ni wasichana wazuri jinsi gani.

52 Nami nakumbuka asubuhi hiyo kundi dogo la Kipentekoste kutoka hapa juu kaskazini mwa nchi, huko

Michigan mahali fulani, wasichana hao walisimama pale wakati Ndugu Hooper ... Nilimwona hapa hivi majuzi usiku, mimi ... huenda asiwe hapa sasa, Ndugu Ed Hooper. Uko hapa, Ndugu Ed? Sidhani yeye ... Aliketi hapa usiku uliopita. Hakuna ... Wengi wenu mnamjua. Yeye na mimi, na Ndugu Hooley, tulikuwa tunaondoka. Na hao wasichana waliosimama pale pembeni wakiuimba huo, walitupa, kila mmoja, ua la waridi ya manjano waliyotoa kwenye nywele zao. (Hapo ndipo yule mwenda wazimu alipoponywa kule chini, mambo makuu yalikuwa yametukia.)

Nilipokuwa nikija barabarani huku nikiwa mwenye furaha nilivyoweza kuwa, mara kikanitokea; mwaka mmoja baadaye kabla sijarudi uwanjani tena, nusura kiniue.

53 Tangu nilipokuwa mvulana mdogo, daima nilisema sikujua ono lilikuwa ni nini. Mvulana mdogo, kila mara nilisema, "La—laiti ningalishikwa na huo usingizi mzito, na kumwona huyo, ningepata afya." Wakati huo ... Daima nilitaka kwenda kwa Mayo kujua shida ilikuwa ni nini. Madaktari kule ...

Tumbo langu huniuma; na loo, jamani! Ndugu Jack alinisaidia kuzunguka nyumba. Ninazunguka moja kwa moja nyumbani; na kama tu maji ya moto yenye grisi, yakiruka kutoka kinywani mwangu. Na kwenda mimbarani, na kuwaombea watu waliokuwa wagojwa maradufu, nao wanaponywa. Wao wameiweka mikono yangu juu ya mtu aliyekuwa na kansa usoni mwake, na hiyo kansa ikaondoka usoni mwake, akisimama pale; nami nilikuwa mgonjwa sana singaliweza hata kusimama.

54 Nanyi hamjui jinsi nimeteseka; mkandamizo wa akili. Kila baada ya miaka saba umekuja, maishani mwangu mwote. Hapo ndipo nilipo sasa, saba nane.

Kwa hiyo nilikuwa—nilikuwa na wasiwasi sana; Nililia, nikaomba, nikasihi.

Nami nakumbuka wakati hatimaye nilifikiri nilikuwa na pesa za kutosha kwenda Mayo kwa ajili ya uchunguzi; wao walisema, "Wao watapata shida yako ni nini." Mimi na mke wangu, na Becky kule nyuma ... Sara alikuwa kitoto kichanga, mdogo sana. Nilikuwa nimeingia tu katika huduma yangu ya uponyaji. Nasi tukaenda kwa Mayo.

Nilipitia kliniki. Na ule usiku uliotangulia...ningefanyiwa uchunguzi wa mwisho asubuhi iliyofuata, niliamka tu na nilikuwa nimeketi pale kitandani nikitazama huku na huko. Nami nikaangalia mbele yangu, na kulikuwa na mvulana mdogo, aliyefanana tu na mimi, mwenye umri wa miaka saba hivi; na nikamwangalia, na ilikuwa ni mimi. Naye alikuwa amesimama karibu na mti wa kale wa mtoni. Na juu ya mti huo ...

55 Ye yote wenu wawindaji wa kuchakulo anajua unaweza ukaparuzi kijiti kwenye mti kama huo hivyo, nako kutamstusha kuchakulo na kumfanya atoka humo kama yumo katika hilo shimo.

Nami nilikuwa nikiona pale ambapo yule kindi alikuwa, nami nikawaza, "Huyo ni kuchakulo wa aina gani?" nami nikasugua. Na nilipofanya hivyo, nilitazama na ilikuwa ni mimi wakati huo mwenye umri wa miaka thelathini na minane, yule mvulana mdogo alikuwa ameondoka. Kwa hiyo nikasugua tawi hilo, na kutoka kwa gogo hilo lenye shimo, mti, akaja kuchakulo mdogo yapata urefu huu, mweusi kidogo, na ilionekana kama mawimbi madogo yalikuwa yakitoka kwake; mwenye macho madogo yenye kung'aa sana, kitu kiovu sana nilichopata kuona, alionekana zaidi kama cheche kuliko kuchakulo.

56 Naye akaniangalia moja kwa moja. Nami nikafungua kinywa changu kusema, "Vema ..." Na nilipofanya hivyo, yeye ... Kabla hujaweza kupepesa jicho lako, akaruka moja kwa moja mdomoni mwangu, akaingia tumboni mwangu, na kunirarua tu vipandevipande. Na nilipokuwa nikitoka kwenye lile ono, nikiwa nimeinua mikono yangu, nikiangalia, nilienda nikalia kwa sauti, "Ee Mungu, unirehemu! Ananiua!"

Nikasikia Sauti huko chini kabisa chumbani, ikisema, "Kumbuka, ina urefu wa inchi sita tu."

Ni wangapi wameisikia hadithi hiyo? Nimewaambia jambo hilo mara nyingi, watu walio karibu na Maskani.

Vema, ikaendelea na kuendelea, nikiteseka vivyo hivyo.

Mayo Brothers, kesho yake, walinichunguza. Kasema, "Baba yako alikuwa Mwairishi, alikunywa pombe. Mama yako akiwa nusu Mhindi, hilo linakufanya uwe karibu mtu aliyechanganya damu. Kwa hivyo utakuwa...wewe ni—wewe ni mtu mwenye fadhaa sana hata haitakuacha kamwe." Kasema, "La sivyo, una afya njema. Lakini hilo, hilo ni jambo fulani katika nafsi ambalo mwanadamu hawezi kulizuia." Kasema, "Utaninii ..." Kasema, "Mtu anapokufa, hiyo haiwezi kufanyiwa uchunguzi wa maiti, maana nafsi yake imeondoka." Akasema, "Vema, hutaweza kamwe."

57 Naye jamaa huyo akasema, daktari wangu mzee, kasema, "Baba yangu alikuwa nayo, alikufa akiwa na umri wa miaka themanini na mitano, tisini," mahali fulani pale, alisema. Kisha akasema, "Mwezi mmoja ama miwili kabla hajafa, nilimchunguza; alikuwa nayo maishani mwake mwote, angevipata hivyo" kasema, "vipindi vya fadhaa."

“Watu wengine,” akasema, “wanapoipata, huwa na hasira ya haraka,” kasema, “hao ndio namna ya watu wanaoweza kukuuu.” Akasema, “Aina ile nyingine, kama wanawake wanapoingia ugumba, wao hulia. Wewe una aina ambayo hujisikia mchofu.” Kasema watu wa kale walikuwa wanaiita, hali ya kuudhika, haingaliwaacha.” Hiyo inapokushika, tumbo lako linakuuma; unahangaika tu.”

Nikasema, “Lakini, bwana, sifanyi kitu.” Nikasema, “Nina furaha.”

Kasema, “Hiyo ni kweli. Hiyo ni nje tu ya mfuko wa vikorokoro vya binadamu.” Kasema, “Utakuwa nayo daima.” Loo, ni jambo la kukatisha tamaa iliyoje!

Lakini hayo maneno, ukiyawazia, “Kumbuka, ana urefu wa futi sita tu,” hayo sijayasahau, kama mke wangu mpenzi kule anavyoweza kuwaambieni. Mwaka baada ya mwaka, nimefikiria jambo hilo.

58 Na kisha, nilipokuwa nikienda ng'ambo wakati huu wa mwisho nilikuwa ... hapo awali. Vema, nilikuwa nimerudi nyumbani, nami nilikuwa kwenye safari ya kuwinda kuchakulo. Nikaruka kutoka katika gari pamoja na Ndugu Banks Wood, ambaye anasikiza usiku wa leo, na nikaanza kupanda kile kilima haraka, na ilionekana kwamba moyo wangu ungenitoka.

Nami nikamwuliza Daktari Sam Adair, nikasema, “Ni kitu gani kinachofanya hivyo?”

Akasema, “Wakati mwingine utakapoipata, chukua kipimo cha moyo.”

Kasema, “Vema.”

Kwa hiyo ikatukia tena katika—mwaka uliofuata, kisha akaenda na kuchukua kipimo cha moyo. Akasema, “Moyo wako hauna shida,” kasema, “wewe una wasiwasi tu.” Ikaanza kuja basi.

59 Vema, daktari mwingine aliniambia, rafiki yangu mzuri, kasema, “Huo ni moyo wako, kijana,” kasema “afadhali uwe mwangalifu.” Huo ndio mwaka niliomwita Ndugu Moore naye akapata mtu wa kuhubiri badala yangu, nilipoenda kuwinda kondoo pamoja na Ndugu Fred. Ningepanda juu ya milima kama nilivyofanya nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, maili baada ya maili, nikikimbia; haikunisumbua hata kidogo. Mnaona?

Nikarudi na kumwambia Sam. Akasema, “Vema, kuna kasoro fulani, afadhali uwe mwangalifu.”

Kisha nikaona ono la daktari mzee amesimama na hao ... daktari mtindo wa kikale akiwa na kifaa cha kuzikilizia mapigo ya moyo, mkononi mwake. Yeye alisema ... Alikuwa amesimama mbele yangu siku moja, akasema, “Usiwaruhusu kukwambia'huo ni moyo wako, 'hulo ni tumbo lako.”

Kwa hiyo, ni—nikawaza, “Vema, nitachukua tu neno hilo, maana lilikuwa ni ono. Njoni.”

60 Nilianza kwenda Afrika; nikadungwa sindano. Ilinipasa kudungwa sindano kadha kabla sijaenda Afrika, hiyo ndiyo sheria. Kwa hiyo, wakati nilipokuwa nikipats hizi sindano, yeye alisema, “Mbona, siwezi kuona kosa lo lote kwako.” Kasema, “wingi wa damu yako, damu yako ni tisini na sita, ni tisini na sita.” Kasema, “Kama ungekuwa na umri wa miaka kumi na sita, isingekuwa yoyote—isingekuwa bora zaidi.” Naye akasema, “Moyo wa kutosha kukufikisha miaka mia moja. Mapafu, kila kitu,” kasema, “uko sawa; hakuna sukari, hakuna kitu.”

Nikasema, “Asante.” Kwa hiyo nikapimwa mwili, na—na kupeleka cheti cha—changu cha afya kwenye halmashauri.

Kwa hiyo, akasema, “Unajua cho chote kuhusu jambo hilo?”

Nikasema, “Sijui kitu ila mwasho usiokwisha tumboni wakati wote.”

Akasema, “Vema, nitakwambia.” Yeye alisema ...

Nikasema, “Loo, nimechunguzwa. Nimekuwa huko Mayo Brothers, na kila mahali.”

61 Akasema, “Lakini ngoja kidogo.” Akasema, “Mara kwa mara kidonda tumboni huwa kidogo sana hata madawa ya kuchunguzia hayawezi kukionyesha; na wakati mwingine ni kikumbwa sana hakiwezi kuonekana, kwa maana X—ray ni kivuli tu. Na kijidonda kidogo sana, huwezi kukiona, hakiwezi kushikika vya kutosha. Vijidonda vingi vinaweza kufanya hivyo.” Akasema, “Namjua daktari mzee humu ambaye amevumbua chombo fulani, wanacho sasa; wanaweza kukufanya ulale kwa dawa fulani kidogo ya magadi, waweke mrija kooni mwako, nao basi hata tumboni mwako waone kuna kasoro gani.” Kasema, “Yeye ...” Kasema, “Yeye ni aina ya watu wako, yeye ni Mkristo.” Kasema, “Mbona usiende kumwona.”

62 Nikachukua jina lake: Daktari Van Ravensworth. Kwa hiyo, niliporudi, nilienda kumwona yule daktari mzee. Loo, yeye ni mzee mzuri kutoka Uholanzi East Indies, kutoka kwenye kundi kubwa la wamishenari. Naye alikuwa amesikia habari zangu na kusoma kitabu changu, na loo, alinipa tu mkono, akasema, “Ndugu Branham, ningefurahi kukufanyia jambo hilo.” Akasema, “Hebu nikwambie utakayofanya; juma

lijalo njoo huku hospitalini," naye kasema, "na unipigie simu kabla hujaenda." Kisha akasema, "Sina budi kukupa pumzi kidogo." Kisha akasema, "Basi nitakapofanya hivyo," kasema, "inakulaza usingizi kwa dakika tano."

Msichana wangu mdogo alikuwa tu amedungwa hiyo ili kung'olewa jino, na msichana mdogo wa Ndugu Norman. "Kulala kwa dakika tano," nikawaza, "hilo haitanisumbua." Kwa hiyo, nilifikiri nitaridhika basi, kuijaribu.

63 Na halafu kesho yake asubuhi, niliamka kitandani na kutazama huku na huko, nikatazama kule kwenye kitanda watu wawili; mke wangu mle, hakuwa ameamka bado. Nami nilikuwa nikiangalia dirishani kuelekea kwenye Milima mikubwa ya Catalina kule ninakoishi, nami nikaangalia kule juu ambapo Malaika wa Bwana aliweka ule Upanga mkononi mwangu, ambapo wale Malaika saba unaowaona kwenye picha walitokea, mambo makuu yaliyotwaliwa mahali.

Nami nikatazama, na nilipotazama, hapo nilikuwa nimesimama karibu na ule mti tena, mahali pale pale yule kindi alipo. Nikatazama huko juu, nikawaza, "Hilo ni tundu la yule kuchakulo." Ndipo nikawaza, "Nikashanaa kama yeye angali yuko huko juu?" katika ono. Nikaparuza kando ya mti, akatoka. Na kabla hata sijapepesa jicho langu ... Yeye alikuwa kuchakuro mwenye sura ya kipekee kuliko wote niliowahi kuona; sasa, itakubidi kujua huduma yangu kujua mifano hii na kadhalika. Alinirikia lakini alinikosa; alikosa kinywa changu, akagonga kifua changu na kuanguka.

Na mara alipofanya hivyo, nikasikia kitu Fulani kikisema, "Nenda kwenye Milima ya Catalina."

64 Kwa hiyo nikageuka, nikasema, "Meda, umeamka, Mpenzi?" Nami nikamwamsha.

Akasema, "Kuna nini?" Yapata saa tano asubuhi.

Nikasema, "Nilikuwa nikitazama hapa nje, nami nikamwona yule kindi tena, Mpenzi."

"Ni kindi gani?"

Nikasema, "Yule niliyemwona kule Mayo." Nikasema, "Unajua nini? Alikosa kinywa changu wakati huu, hakunipiga, alitoka akaenda kifua ni mwangu." Nikasema, "Mungu asifiwe! Nimelitazamia, loo, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, nimetamani kuona jambo hilo likitukia. Kama ningaliweza kuona jambo hilo likitukia, hata ... Kabla sijajua ono lilikuwa ni nini, kama ningeweza kuona jambo hilo likitukia, basi nikasema, 'Ningekuwa mzima. Chochote kile alichoniambia, hivyo ndivyo ningekuwa.' Na kwa miaka arobaini nimetazamia jambo hilo, na hapo likatukia."

Kabla, nilipokuwa kule Mayo, wakati uo huo nilikuwa huko juu waliponipa ujumbe huo, nami nikaona ono ...

65 Mama yangu mzee ameenda Utukufuni sasa, mwanamke wa kipekee sana. Alikuwa na ndoto tatu au nne maishani mwake, nazo daima zilikuwa ni za kweli. Yeye angeniambia, na ninii ... Angeanza kuniambia, ningemwambia ... Ningesema, "Simama moja kwa moja ... Mama, nitakwambia hayo mengine ni nini." Mnaona?

Kwa sababu kila mara unaponipa ndoto ya kufasiri, sikuzote huniambii ni nini hasa. Ndipo ninapoliona tena, ninaona kile hasa ulichokiota, ndipo anianiambia ni nini. Mnaona? Haikulazimu kuniambia ndoto hiyo ni nini, Yeye hunionyesha ndoto Mwenyewe. Mnaona? Na halafu ninaona, ninasema, "Vema, hukuniambia jambo *hili* na kuniambia *vile*." Mnaona? Na kwa hiyo Mungu anayeweza kufasiri ndoto, anaweza kuonyesha ndoto; Anaweza kuonyesha moja, anaweza kulifasiri. Na kwa hiyo basi ...

66 Vema, je! Hakukuwako na kitu kama hicho katika Biblia, kilichosema, "Kama unaweza ..."? Ni—ni ... Ilitokea tu kwamba ilinijia. Danieli, sivyo? La, Yusufu—Yusufu. Vema, iko mahali fulani katika Biblia. Nilikumbuka tu jambo hilo, nikasema, "Kama unaweza kuniionyesha ... Kama unaweza kuniambia nini ..." Loo, ni Mfalme Nebkadreza, hiyo ni kweli. Kasema, "Kama unaweza ... Kama huwezi ..."

Wale wachawi wakasema, "Niambieni ile ndoto."

Akasema, "Umeniacha." Hiyo ni kweli, ya kwamba, ninakumbuka jambo hilo; niliwazia tu jambo hilo basi.

Sasa angalia. Naye Mama, akasema, "Billy," niliporudi, akasema, "njoo hapa, mwanangu, ukaketi." Akasema, "Niliota ndoto ya ajabu. Niliota ya kwamba nilikuona umelala mgonjwa, karibu kufa, na tumbo lako kama kawaida." Yeye amenipikia vyakula vingapi! Naye akasema, "Ulikuwa ukijenga nyumba juu ya kilima." Kisha akasema, "Niliona hua sita weupe wakishuka kutoka mbinguni, wakinong'oneza, katika herufi 'S' nao waliketi kifua ni mwako. Nawe ulikuwa ukiangalia, na yule aliye mbele alikuwa akijaribu kukwambia jambo fulani." Kasema, "Walikuwa wenye kung'aa sana, weupe, hua. Nao wakachukua vichwa vyao vidogo na kuviweka shavuni mwenu, na kwenda, 'ko, ko, ko.'" Kisha akasema, "Sikuweza kufahamu jambo hilo." Kasema, "Waliendelea tu kwenda, 'ko, ko, ko.'"

Nikasema, "Loo, ninaona jambo hilo, Bwana asifiwe!" Na kasema, "Waliunda herufi yao ya 'S' tena na kurudi juu angani, wakienda 'kuu, kuu, kuu, kuu,' wakirudi nyumbani."

Vema, yule mnyama mdogo niliyemwona alikuwa na urefu wa inchi sita. Huo mlolongo wa hua ambao Mama aliuona ulikuwa wa hua sita, sita si kamilifu. Nilijua ya kwamba siku moja ningemwona huyo wa saba. Huyo alikuwa ni mwanadamu, akiteseka; ndivyo ilivyoendelea na kuendelea.

67 Asubuhi hiyo, niliamka baada ya kuona ono hili; Nilimtii Bwana. Nilimpeleka mvulana wangu mdogo, Joseph, shuleni. Yeye ananisikiliza mimi sasa, huko Tucson. Nikampeleka shuleni, na nikamwambia Meda sikujua ningerudi lini.

Nami nikaondoka nikaenda Catalina, juu ya—ya vilima, na—na nikaenda mahali ambapo Malaika wa Bwana aliweka Upanga mkononi mwangu. Mapema kabisa; kisha nikaanza kupanda mlima.

Vema, badala ya kupanda juu kwenye vilele upande huu (ambako kuna nyoka wengi, nge, mnajua jinsi Arizona ilivyo), niligeuka upande wangu wa kulia; Kitu fulani kilisema, "Geuka upande wako wa kulia." Nilikwenda moja kwa moja kwenye vilele; Nilizunguka -zunguka, nami nilikuwa nikizunguka hiyo miamba mikubwa mikubwa, mikubwa mara mingi kuliko maskani haya, nikiwa juu ya vilele vyake pale ambapo ni mara chache mtu angeweza kufika.

68 Na karibu na saa tano, nilikuwa nikienda kwenye pango dogo, huko nyuma mahali fulani ... mahali padogo palipoingia namna hii kwenye njia ndogo ya kulungu. Nami nilikuwa nimevua shati langu, kofia yangu mkononi mwangu, kwa sababu nilikuwa nimelowa tu kwa jasho. Na kwa hiyo nikageuka mle, na nilipokuwa nikiingia kwenye hilo pango dogo, nilihisi uwepo wa Bwana. Nikavua kofia yangu na kuangalia kote. Nikawaza, "Yuko hapa mahali fulani. Ninajua Yeye yuko hapa." Nikawaza, "Ni kitu gani?" Nikapiga hatua chache zaidi. Nikasema, "Bwana, Wewe uko hapa mahali fulani."

Nami nikaangalia kule kando ya njia, na huyo maskini kuchakulo amelala; alikuwa amerukia kitu fulani na kukikosa, na akagonga kijiti cha mpungate (huo ni mpungate urukao). Kilijishindilia kichwani mwake, kifua, tumboni, naye kafa. Yule maskini kuchakulo wa sura ya ajabu, alikuwa amekosa kinywa changu na kuugonga huo mpungate. Nayo Sauti ya Bwana ikasema, "Adui yako amekufa." Nilisimama pale, nami nikatetemeka. Nilichukua mguu wangu na ku- ...

69 Kwa kawaida kunguru wangekula. Nilimwua nyoka, siku kadhaa baadaye, alilala barabarani yapata nusu saa. Daima kuna tai na kunguru wanaoruka kupitia huko, nao watamchukua sasa hivi. Nalimwua nyoka wa matumbawe, huyo ndiye nyoka hatari sana tuliye naye; alikuwa amelala karibu sana nami; siku chache baadaye. Nikaanza kurudi kumchukua nikamwonyeshane, kunguru walikuwa tayari wamemchukua, ndege waliokuwa wakipita pale.

Na huyo ilikuwa imekaa pale tangu nilipokuwa nimeona lile ono, siku mbili zilizopita; Ninaamini ilikuwa Jumamosi, nami nilienda kule Jumatatu. Kwa hiyo huyo hapo, amelala pale amekufa. Nilimponda kwa mguu wangu.

70 Nikarudi huku na huko, nikaketi chini tena; niliketi pale na kulia kwa muda, kisha nikaomba; nikiangalia huko chini Tucson, maili kadhaa chini yangu.

Nikageuka na kurudi, angali alikuwa pale. Nilipoingia kwenye pango hilo Roho wa Mungu alikuja juu yangu tena.

Nikazunguko kote, nikashuka mlimani. Nikaingia na kumwambia mke wangu, nikasema, "Mpenzi, sijui jinsi gani, lakini nitapona."

Dk. Ravensworth, aliponifanyia uchunguzi, alisema, "Haiwezekani kabisa kwako kuwa mzima." akanidunga ile sindano ya dawa yenye magadi ambayo ingalinichukua muda wa dakika tano, nami nikalala masaa kumi. Kwa hivyo kitu hicho, hata asprini hunibwaga chini. Kwa hiyo wao ... Akanidunga sindano, akatia huo mrija kooni mwangu. Nilipokuja, naye akaniambia kesho yake asubuhi, akasema, "Kasisi, nachukia kukwambia jambo hili, lakini" kasema "kuta za tumbo lako hata ni ngumu sana, zimekauka." (Sikuziona; alitumia jina la gastritis, nami nilienda na kuliangalia kwenye kamusi na ilisema, "kitu ambacho kimenyauka kabisa"). Kisha akasema, "Huwezi kupona." Yeye alisema, "Utakuwa nao daima." Nami ningalikuwa mtu aliyevunjika moyo kama isingalikuwa ni kwa ono la Bwana.

71 Na kesho yake Kitu fulani kikasema, "Rudi mlimani."

Na siku hiyo badala ya kwenda njia moja, niliongozwa kwenda njia nyingine. Nami nilikuwa nimesimama pale; na nilipotazama, hapo mbele yangu, alikuwa yule hua mdogo mweupe, akinitazama. Nilipangusa macho yangu, nikasema, "Hakika, ni ono; bila shaka." Nikaangalia, nami nikasema, "Ewe hua mdogo, unatoka wapi?" Ni mrembo tu na mweupe, huenda angekuwa ni njiwa; cho chote kile, huko mbali huko jangwani.

Mungu Mwenyezi, aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu, ambaye mimi ni mtumishi Wake, na Neno Lake

likiwa hapa, limefunguliwa mbele zangu, anajua ya kwamba nasema kweli wala sisemi uongo.

Huyo hapo hua ametua, amekaa pale akiniangalia. Nilitembea huku na huko, nikawaza, "Hakika, ni ono." Nikageuza kichwa changu, nikatazama kule nyuma, naye alitua pale, hizo mbawa ndogo, zilikuwa nyeupe kama theluji iwezavyo kuwa; miguu yake midogo, na ya kimanjano; na mdomo wake mdogo wa kimajano; ametua pale huku ananitazama. Alikuwa akiangalia moja kwa moja upande wa magharibi. Nikamzunguka namna hiyo, nisingemgusa kwa cho chote. Nikafuata huo mkondo; nikatazama nyuma, alikuwa pale bado anitazama.

Ndugu, kama mwana wa Ibrahimu, sijali yale daktari aliyoniambia, nitakuwa mzima, hata hivyo!

72 Siku ya tatu nilirudi, nilikuwa nikipanda juu sana. Na wengi wenu mnajua ono kuhusu chifu wa Kihindi akipanda farasi kwenye ule ukuta mdogo kuelekea magharibi. Kitu fulani kilinivutia kwenye mwamba mkubwa, yapata aduhuri, kasema, "Weka mikono yako juu ya huo na uombe." Mungu Mbinguni anajua hii ni kweli.

Niliweka mikono yangu juu ya mwamba na kuangalia juu Mbinguni na kuanza kuomba. nikasikia Sauti ikitoka juu ya hiyo miamba pale, kasema, "Unaujegemezea nini, moyo wako?" Nami nikainuka nyuma namna hii, mabega yangu wazi; uchi kutoka kiunoni kwenda juu, joto. Nikaangalia nyuma. Nikatazama nyuma. Na ilikuwa imeandikwa kwa kito cheupe, kwenye jiwe, "Tai Mweupe," kile lile ono lilisema kingelela Ujumbe wa pili.

Nikajawa na furaha sana, nikakimbia nyumbani; nilikachukua kamera na kurudi kesho yake, na kuipiga picha. Ilikuwa ingali pale, imeandikwa katika mwamba: "Tai Mweupe." (Njiwa akimwongoza tai.)

73 Kwa namna fulani, na—najua. Nitawaambia kabla halijatukia. Daktari ni daktari mzuri ... daktari mzuri, hapana shaka; Na—nafikiri yeye ni mtu mzuri. Lakini na—najua nitapona. Imekwisha! Imekwisha, nami nitakuwa mzima!

Nami nilikuwa nikiwazia wakati Ernie alipoimba wimbo huo muda mchache uliopita, Juu ya Mbawa za Hua. Je! Sauti yake ikoje? Nianzishie, Ernie.

... Mabawa ... hua mweupe kama theluji, (imbeni pamoja nami)  
Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
Ilikuwa ni ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua.

Nafahamu Ernie alitengeneza aya mbili za hiyo. Nitawafanyia vifungu vitatu.

Nuhu alikuwa alichukuliwa  
Juu ya mafuriko siku nyingi,  
Alitafuta nchi kavu,  
Kwa njia mbalimbali;  
Shida alizokuwa nazo,  
Lakini si kutoka juu,  
Kwa kuwa Mungu alimpa ishara Yake  
Juu ya mbawa za hua.  
Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
Ilikuwa ni ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua.  
Yesu, Mwokozi wetu  
Alikuwa duniani siku moja;  
Yeye alizaliwa katika hori,  
Katika hori la nyasi kavu;  
Ingawa hapa alikataliwa,  
Lakini si kutoka juu,  
Kwa kuwa Mungu alitupa ishara Yake  
Juu ya mbawa za hua.  
Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
Loo, ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua.  
Ingawa nimeteseka  
Kwa njia nyingi,  
Nililia kwa ajili ya uonyaji  
Usiku na mchana;  
Lakini imani haikusahauliwa  
Kwa Baba aliye juu,



Yeye alinipa ishara Yake  
 Juu ya mbawa za hua.  
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Loo, ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.  
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

74 Mungu mpenzi, ninakushukuru kwa ajili ya mambo haya, Baba. Ulimpa Nuhu ishara, uliupa ulimwengu ishara, nawe ukanipa ishara. Na kesho yake, nikimwona yule tai akiruka, Ee Mungu, kuna Ujumbe unaokuja sasa, nami naomba, Mungu, ya kwamba utamwacha Hua aongoze. Tujalie, Bwana. Imeniongoza kwenye imani ambayo sikuwa nayo hapo kabla. Ninajua, Mungu, ninajua itakuwa sawa; kwa hiyo ninakushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Baba.

Na, usiku wa leo, tuma Ujumbe Wako tena, Bwana, juu ya mbawa za Hua wa Neno. Tujalie, Baba mpendwa wa Mbinguni. Na kila mtu anayepitia kwenye jukwaa hili, usiku wa leo, na huko nje kwenye mikutano kote nchini, jalia Hua wako mkuu wa imani aingie mioyoni mwao na kuwapa imani, Bwana, kwa ajili ya uponyaji wao. Kumbuka ya kwamba Mungu hana upendeleo. Angeweza kupeleka Ujumbe kwa Nuhu, angeweza kuutuma kwa Yohana Mbatizaji, angeweza kuutuma kwangu, anaweza kuutuma kwa wengine.

Ninaomba ya kwamba huyo Hua ataruka ndani ya kila moyo sasa hivi, Bwana, kwa mdomo Wake mdogo wa dhahabu, na kunong'oneza kwamba, "Kwa mapigo Yake ... Kwa majeraha Yangu na kupigwa Kwangu mmeponywa." Mungu, jalia ya kwamba makosa yetu yatafutwa, maovu yetu yatasamehewa, na kwamba magonjwa yetu yataponywa. Liko mikononi Mwako, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Huku vichwa vyenu vimeinamishwa kwa dakika moja zaidi.

75 Ni wangapi hapa wangetaka kusema, kama mnaweza na mnataka kusema jambo hili, "Ndugu Branham, nimekuwa nikikosea maisha yangu yote. Nimetaka kumtumikia Mungu, lakini usiku wa leo niko tayari kujisalimisha. Mwombe Mungu, ya kwamba huyo Hua ataruka moyoni mwangu usiku wa leo. Ninaweza kumsikia akipepea mabawa Zake anapoingia"? Inueni mikono yenu, sivyo? Hapa katika kusanyiko linaloonekana, jamani, kote jengoni.

Huko mbali kabisa katika wasikilizaji kote nchini, huko juu kwa Ndugu Hunt na Ndugu Coleman, hadi kwa Ndugu Leo na hao wengine, huko chini Tucson, kule kwenye Maskani ya Branham, kote Pwani ya Magharibi, inueni mikono yenu kila mahali: "Ninamtaka Hua kuruka moyoni mwangu usiku wa leo. Nilettee upendo mtamu wa Mungu juu ya mbawa za Hua mweupe kama theluji, Roho Mtakatifu. Nilettee, usiku wa leo, Bwana, na uingie moyoni mwangu imani ninayohitaji."

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba, Mungu, tusamehe dhambi zetu. Hua aliyejeruhiwa amerudisha Ujumbe, Ee Mungu, "Imekwisha!" Tunaamini jambo hilo. Tupe tu imani ya kuliadini, tunaomba. Katika Jina la Yesu. Amina.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Ilikuwa ni ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

76 Huyo hua alitoka wapi? Sijui. Asingekuwa huko nje huko nyikani namna hiyo. La, la! La, asingekuwa kule. Na kwa nini alikuwa mweupe? Baba wa Mbinguni anajua alikuwa mweupe kama shati langu. Huyo hapo ameketi pale.

Lakini ilikuwa juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Loo, ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.  
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Loo, ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

Loo, hivi hamjisikii wanyenyekevu sana? Hebu na tupeane mikono, na tuuimbe.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

Hebu na tumwinulie mikono yetu, na kuuimba.  
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.  
 Nuhu alikuwa amechukuliwa  
 Juu ya mafuriko siku nyingi,  
 Alitafuta nchi kavu,  
 Kwa njia mbalimbali;  
 Shida alikuwa nayo,  
 Lakini si kutoka juu,  
 Mungu alituma ishara Yake  
 Juu ya mbawa za hua.  
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alituma upendo Wake safi, mtamu,  
 Loo, ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.  
 Yesu, Mwokozi wetu  
 Alikuwa duniani siku moja;  
 Alizaliwa katika hori,  
 Katika hori la nyasi kavu;  
 Ingawa hapa amekataliwa,  
 Lakini si kutoka juu,  
 Mungu alitupa ishara Yake  
 Juu ya mbawa za hua.  
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

77 Mbona, mimi mzee, niliteseka maisha yangu yote, kwa nini aliniponya sasa? Ninaamini nitapanda njia hii tena, sina budi kuleta Ujumbe! Nami ninamwambia Baba yangu, usiku wa leo, (kama Junior alivyoona katika—katika ndoto usiku mwingine wa mbawa za huyu Hua, akitembea kwenye madirisha haya hapa), Bwana, mtumishi Wako anaripoti kwa ajili ya huduma. Amina, niko tayari!

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu hunitumia upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

Hebu na tuamini sasa ya kwamba Yeye anaingia juu ya wasikilizaji.  
 Juu ya mbawa za nyeupe kama theluji ... (Tunangojea, Bwana.)  
 Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

78 Ninyi mlio na kadi za maombi, katika marefu haya ya kanisa hapa, sogeeni mbele hapa; simama, songa mbele katika marefu haya hapa, upande huu.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

Wale walio na kadi za maombi katika mstari huu, njoni upande wa kushoto.  
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu hutuma upendo Wake mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

Hao ... [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]  
 Loo, juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
 Mungu alinitumia upendo Wake safi, mtamu,  
 Ishara kutoka juu,  
 Juu ya mbawa za hua.

79 Yule hua alitoka wapi huko nyikani? Ningesema jambo hili: Mungu aliona Ibrahimu alihitaji kondoo dume kwa ajili ya ishara, Yeye ni *Yehova-Yire*, "Bwana anaweza kujipatia sadaka Mwenyewe." Kufikiria jambo hilo! Mungu yeye yule, kwa uvuvio ule ule, kwa watu wa aina ile ile, alituma hua. Yeye angali ni

Mungu, Yehova-yire anaweza kutoa chochote anachohitaji.

Mbona wewe, wakati tu unapopitia mstari huu wa maombi, usimuulize Mungu akupatie juu ya mbawa za Hua? Huyu Hua, Roho wa Roho Mtakatifu, akupe imani moyoni mwako upate kuamini ya kwamba utaponywa.

80 Ninajaribu kuwafanya wote wasimame, mnaona. Ninaomba sasa. Ndugu Brown yuko mahali pake. Ndugu Jack ... Unasemaje? [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham — Mh.] Sawa kabisa, vema. Sehemu *hii* hapa, inakuja kupitia huku kwanza, ambayo imepangwa. Sehemu *hii* hapa, itapitia upande *huu* kwanza, ambao wamefanya mstari. *Hawa* watafuatia upande huu. *Nanyi* mfuata hawa hapa, mkija moja kwa moja humu mkaombewe.

Sasa, nina hakika huu hautakuwa mstari unaoenda kwa haraka, tutachukua muda kidogo tuweze hasa kumwombea kila mmoja, tuwezavyo.

Sasa, nilifupishaujumbe wangu kidogo (nanyi nyote mliupata huo, mnaona) kusudi nipate mstari huu wa maombi. Huu ni mstari wa kumbukumbu ya heshima ya siku ambazo Ndugu Jack Moore, Ndugu Young Brown, wake zenu waliwaruhusu kwenda, nanyi mkaja na tukaingia California, na kote katika Arizona (Pamoja, kupitia jangwani) na kuombea wangonjwa.

81 Unajua nini? Kuna watu wanaoishi leo ambao walikuwa wakifa wakati huo, na wangali hai kwa sababu ya jitihada hizo. Ilifanyaje? Ikaleta uponyaji wa Kiungu katika kila kanisa lililomo nchini, sasa hata Wapresbeteria na kadhalika. Wao ... Ilinyamazisha midomo yao, kwa sababu ilimhitaji Mungu kumtia mafuta mtu fulani apate kumua Goliathi, kuonyesha ya kwamba ingeweza kutendeka, ndipo wengine wao wakajipa moyo (hiyo ni kweli) na wakasonga mbele. Inaweza kufanywa tena, kwa maana Yeye angali anatuma upendo Wake juu ya mbawa za Hua.

Wakristo, ninawatakeni msikilize. Kama ningeweza kusimama hapa na kujaribu kuwanukulia mambo ya kimbinguni ambayo nimeona yakitendeka hata katika miaka mitatu iliyopita, ningekuwa hapa wakati huu Jumamosi ijayo usiku, nikiwaambia. Hata sizungumzii jambo hilo sana, maana inasikika kana kwamba haiwezekani, bali ninawaambia Kweli. Ni Kweli kabisa. Tunaishi chini ya uongozi wa Yehova Mwenye Nguvu, yule yule aliyekuwa pamoja na manabii katika Agano la Kale, pamoja na Kanisa katika Agano Jipya, Yeye yuko hapa leo akimchukua Bibi -arusi kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake. Liamini! Hivi hamtafanya hivyo, enyi watu? Kama uliwahi kuliadini, liadini sasa hivi. Huyu ndiye ambaye ... Ninawatakeni mfanye hivyo. Hatujui yatakayotendeka bado usiku wa leo. Hatujui kitakachotukia. Tunangojea tu chini ya matarajio.

82 Tafadhali, katika Jina la Bwana Yesu, nawaomba kama mtumishi Wake. Ninajua mnaposhughulika na kusanyiko, mna kila kitu kilichochanganyikana mle. Lakini kama uniamini mimi kama mtumishi Wake, kama kuna shaka moja (au dhambi ni—ni "shaka, kutokuamini"), kama kuna chembe moja ya jambo hilo moyoni mwako, mwombe Baba aiondoe sasa hivi. Mnaona? "Bwana ..." Na ndipo utakapokuja na imani halisi ... Sasa, mikono yangu haitamaanisha kitu isipokuwa Hiyolikuguse wewe kwanza; ndipo itakapokuja, itaiangazia, nawe utaponywa. Hiyo ni kweli, utajua utaponywa. Unaona, utaiadini.

83 Sasa, nitaomba sasa kwa ajili ya kila mmoja wenu. Na sasa ... Mnapofanya jambo hili, mnawekeana mikono ninyi kwa ninyi, kwa hiyo tunanini ... Nawe utakuwa ukimwombea mtu uliyemwekea mikono, ndipo nitawapitisha kwenye mstari. Weka mikono yako juu ya mtu aliye pamoja nawe kwenye mstari.

84 Mungu mpenzi, si—sijui njia nyingine ya kusema mambo haya, Bwana. Ninajua tu kusema yale ninayojua ni Kweli, na Wewe ni shahidi wangu usiku wa leo kwamba ninasema Kweli. Imani yangu, Bwana, na uponyaji wangu mwenyewe katika siku za usoni; Sijui ni lini, sijui ni namna gani, sielewi; bali ninaamini jambo Hilo, Bwana, ya kwamba niliipokea ile ishara kutoka juu. Huyu hua wa saba hatimaye alifika humu, ile inchi ya saba imetimilizwa hivi karibuni kwa huyo mnyama. Imekwisha!

Mungu, ninataka kuwatumikia watu Wako. Kwa hiyo ninaomba, Mungu, ya kwamba utatutia mafuta sana usiku wa leo ili kwamba yeyote tutakayemwekea mikono, jalia waponywe; si kwa sababu ni sisi, bali ni kwa sababu inafuata amri Yako. Ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Bwana, nisaidie kuamini, na usaidie mioyo yao iwe kitalu cha imani. Na hebu, pamoja, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kila mtu mgonjwa na anayeteseka katika jengo hili (ama majengo kote nchini) anayetii amri hizi sasa, ataponywa. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

85 Iweni na imani; nyote ombeni pamoja nasi. Sasa, huu si mstari wa upambanuzi.

[Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Huzuni, hofu, ninajua nini hii ... [Huyo dada anazungumza na Ndugu Branham.] Maskini mwanamke huyu, alisema yeye hajaona amani maishani. Jambo lile lile ambalo mimi ... hawezi kulala anashikwa na fadhaa, ana wasiwasi.

Mungu mpendwa, nishuhudie, Bwana, ya kwamba nimesema Kweli. Namna ninavyojisikia kwa ajili ya maskini mwanamke huyu! Ninaomba, Mungu, ya kwamba utamtumia, usiku wa leo, ule mwali wa imani

kutoka juu ambao unajua ya kwamba Wewe unawajibika kwa Neno Lako, nawe utatimiza kila Neno. Mungu wa Mbinguni na aondoe hofu hii kutoka kwa dada yangu. Nami nakutii kwa kumwekea mikono na kuhukumu. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia litoke kwake. Amina.

Sasa, angalia dada, unaniamini sasa, kama unaweza kuanza kutoka papa hapa, kwa msalaba. Tangu usiku huu, kanusha ya kwamba una jambo hilo. Waona, endelea kusema, "Sina huo tena." Kisha utakuacha.

86 Dada Palmer. [Dada Palmer anazungumza na Ndugu Branham — Mh.] Naam. Dada yetu, Dada Palmer; mumewe ni rafiki yangu mpendwa sana, mhudumu kutoka Georgia ama Alabama, Georgia—Georgia. Naye alikuwa akija maskanini ... Wao huendesha gari, ninapohubiri huko maskanini, maili elfu moja na mia tano kusikiliza ibada moja. Ndugu Palmer alishindwa kulidhibiti gari lake, ama yule mvulana, mmoja, walipokuwa wakipiga kona, nao wakaanguka. Yeye ana madhara yake.

Hebu na tuombe.

Mungu mpendwa, mponye huyu mtumishi Wako, maskini mke wake, mwaminifu, wa kweli, mtumishi mdogo katika Kristo, naomba, Mungu ninapomwekelea mikono yangu pamoja na Ndugu Jack Moore hapa, ya kwamba utamponya na kumpa afya. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki! ...?...

87 Katika mguu wa kuume, nawe unasimama kwa ajili yake? Mvulana wake mdogo ni mlemavu, naye anaumwa na tumbo lake na mgongo pia.

Hebu na tuombe.

Mungu mpendwa, na huyo Hua mweupe kama theluji aingie kwenye kilindi cha moyo wake sasa, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Ninaomba jambo hili liwe hivyo kwa ajili ya ndugu yetu na kwa mwanawe mdogo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ma maumivu makali ya kichwa, na maradhi ya mguu yanayomsumbua wakati anafanya kazi.

Mungu mpenzi, jalia baraka Yako ya uponyaji juu ya kijana huyu, tunapomwekea mikono yetu kama watumishi wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

88 Yeye yuna shida ya wanawake, kike, na pia anataka ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Mungu mpendwa, ninaomba maombi haya ya imani kwa ajili ya maskini bibi huyu, na shida hiyo ya kike iondoke, hebu ubatizo wa Roho Mtakatifu uje juu ya mbawa za Hau, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada.

Ukuaji kwenye jicho lake, na kwa rafiki yake mwenye upendo.

Mungu mpendwa, unajua mioyo ya wanadamu. Ninakuomba Baba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utatujalia ombi hili ambalo ndugu huyu ameomba; na kutii kwetu Neno Lako la kumwekea mikono. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, ndugu.

Ana uvimbe katika upande wake wa kushoto, na pia sauti yake ni mbaya.

Mpendwa Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya dada huyu; nikiweka mikono yangu juu yake katika Jina la Yesu Kristo, ili uponyaji wake uwe. Amina.

Mungu akubariki, dada yangu.

Bila shaka, dada, ninaona shida yako, kiungo kilichovimba. [Huyo dada anazungumza na Ndugu Branham — Mh.] Figo, kibofu cha mkojo, na kifundo cha mguu vimetupwa mahali pake.

Ee Baba, Mungu, mponye mwanamke huyu wa thamani, Bwana, ninaomba, ninapoweka mikono yangu juu yake katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada; Hiyo ndiyo njia, itafanywa.

Mnasikia hilo, sivyo, kwenye maikrofoni? Yeyote aliye kwenye ... mhandisi, kama utaiimarisha kidogo tu, wasikilizaji wanaweza kusikia ushuhuda wao ... ama yale wanayosema wanapokuja. Waombeenii mnapousikia; ninapoanza kuomba, ombeni pamoja nami.

Mungu mpenzi, ninamwomba huyu dada yetu, ya kwamba utamponya, Mungu mpendwa. Tunafanya

jambo hili kwa sababu ni amri Yako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, dada.

89 Mungu mpenzi, unasikia ushuhuda huo, unasikia yale adui amemtendea. Tunajaribu kuchukua Jina la Yesu na kumshinda adui huyu; Yeye yuko tayari kwa sababu Hua aliyejeruhiwa, mwenye milia alianguka sakafuni mwa Nyumba ya Mungu akiwa na Ujumbe, "Imekwisha!" Tujalie, jalia aamini jambo hilo, Baba, katika Jina la Yesu.

Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya huyu dada yetu. Jalia Hua wa Mungu amshuhudie usiku wa leo ya kwamba Yeye alimfanyia jambo hilo, apate kuwa mzima. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya ndugu yangu anayesimama hapa. Alikuwa na imani ya kutosha kufika umbali huu, Bwana, sasa jalia apokee uponyaji wake na aende kwenye kiti chake akiwa mzima. Katika Jina la Yesu.

Mungu mpenzi, ninamwomba ndugu yetu, nikimwekea mikono. Saidia, Mungu mpendwa, ya kwamba imani ya Mungu itazama chini wakati huu; na kuwa kama Ibrahimu, kuyaita mambo hayo yaliyoko, kana kwamba si—hayapo, kwa maana Mungu alifanya ahadi. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki.

90 Mungu mpenzi, Wewe ndiwe unayeweza kufanya uamuzi wa kweli. Ninaomba, Mungu mpenzi, kama vile msichana huyu aliomba hili, jalia apokee katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya dada yetu katika kutii yale uliyosema tufanye. Hii inaturudisha nyuma kwa miaka mingi, Bwana, kwa kuwa tunaendesha mstari wa maombi namna hii; bali tunajua kilichotukia wakati huo, tunajua Wewe ni Mungu yule yule leo kama watu wanaweza kuwa na imani ile ile leo. Ninaomba katika Jina la Yesu kwa ajili ya uponyaji wa dada yetu. Amina.

Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya ndugu yangu hapa na kuomba uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Baba, ninamleta mbele Yako usiku wa leo huyu dada yetu, na kuweka mikono yangu juu yake kushuhudia ya kwamba ninasimama kama shahidi wa nguvu Zako, ninasimama kama shahidi wa maono Yako, Neno Lako, nami ni shahidi kwamba Wewe ni Mungu. Nami ninaweka mikono yangu juu yake katika kutii Neno la Mungu wangu, na kuomba aponywe. Amina.

91 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya ndugu yangu vivyo hivyo, kama shahidi wa nguvu Zako ninaomba aponywe katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] "Nini?"

Akasema, "Mponyaji." Kasema ya kwamba "Mtu fulani kutoka mahali fulani, huko Arkansas, alikuwa ameponywa asubuhi hiyo, kipofu anayetengeneza viatu." Mnajua hadithi hiyo. Ingekuwa kwenye redio.

Nami nikasema ... Nikawaza ... Nilicheza sehemu ya mnafiki. Nikasema, "Huamini hiyo ni Kweli?"

Akasema, "Naam, bwana, ninaamini."

Nami nikasema, "Je! Unaamini katika siku hii ambapo Mungu angefanya kitu kama hicho, wakati ..."

Akasema, "Bwana, nilisikiliza kipindi cha kidini." Akasema, "Mimi ni Mkristo." Akasema, "Nalisikiza vipindi hivyo, nikamsikia huyo mtu kule aliyeponywa asubuhi hii, huyo kipofu mtengenezaji viatu. Walimtupa nje ya kanisa, alikuwa akipiga makelele sana, kanisa moja hadi lingine. Akiwa na kofia yake juu ya fimbo, akiizungusha huku na huko, akienda huku na huko makanisani, kila mtu mjini, akipaza sauti, 'Nimeponywa! Nimeponywa!' Kipofu mtengeneza viatu."

Nikasema, "Je! Unaamini jambo hilo?"

Naye akasimama pale kidogo, kulikuwa na manyunyu ya mvua, akasema, "Bwana, ukinipeleka mahali aliko, ndipo nitamwona Baba yangu." Ndipo nikajisikia namna hiyo.

Nikasema, "Labda mimi ndiye unayemtafuta."

Akasema...akanishika ghafla kwenye kunjio la koti langu kifuni, akasema, "Wewe ndiye huyo mponyaji?"

Nikasema, "La, dada, lakini mimi ni Ndugu Branham."

Akasema, "Unirehemu!"

Nikawaza juu ya maskini kipofu wa kale Fanny Crosby, "Unapowaita wengine, usinipite." Mnaona,

Yeye alikuwa amemponya mmoja, angeweza kumponya yeye.

Nikaweka mikono yangu juu ya macho yake, nikasema, "Yesu mpendwa, siku moja msalaba wa kale usio laini ulikuja ukifanya vishindo barabarani, mabega yakitoka damu, mwili huo mnyonge ambao ulianguka chini ya mzigo huo. Mtu mweusi jina lake Simoni, wa Mkirene, alikuja na kuuchukua msalaba, akamsaidia kuubeba. Nina hakika unakumbuka jambo hilo, Baba. Na mmoja wa watoto wake anashangaa hapa gizani, nina hakika unafahamu."

Akasema, "Utukufu kwa Mungu! Ninaweza kuona!" A-ha.

Nikasema, "Waweza kuona?"

Akasema, "Naam, bwana."

Nikasema, "Hesabu hizo taa." Naye akawahesabu. Nikasema, "Nimevaa suti ya rangi gani?"

Kasema, "Umevaa suti ya kijivu, na tai ya manjano." Hilo ndilo, angeweza kuona.

Loo, Mungu huheshimu unyenyekevu. A-ha.

*Na hili lenyewe ndilo litakalosababisha, na kutimiliza, ule ushindi mkuu katika Upendo wa Kiungu.*

Mungu mpenzi, mrehemu na umponye dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

92 Mungu mpenzi, ninapouchukua mkono huu mnyonge, wenye makunyanzi, Wewe tu ndiye unajua yaliyopitia hapa. Ninaomba, Mungu mpendwa, ya kwamba mkono ule ule nilionao usiku wa leo utakumbatia kama hiyo mikono dhaifu ya Simeoni siku hiyo, "Bwana, jalia mtumishi Wako aondoke kwa amani, kwa kuwa sasa nauona wokovu Wako." Jalia lije juu yake, Bwana, wokovu Wako, na kumfanya mzima katika Jina la Yesu. Amina.

93 [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Kuhusu "Ile Hukumu, Bw. Kutokuamini alimshtaki Yesu Kristo. Mnakumbuka ile Kesi? Namna ambavyo ninii ... Walikuwa na ma—mawakili na kila kitu, na ni nani aliyemtetea. Nasi tulikuwa na mw—mwendesha mashtaka, Shetani, ambaye alikuwa anaenda kushtaki; namna ambavyo, kesi ilivyoletwa.

Naye akasema, mmoja, Bw. Doubter, akaja, akasema, "Nilimsikia mhubiri akisema, 'Wapake mafuta wagonjwa, Biblia inasema hivyo.' Nilikuwa nimepakwa mafuta, sikuponywa. Huyu mwingine alisema, 'Weka mikono yako juu ya wagonjwa, watapata afya.'" Alikuwa akijaribu kushtaki.

Lakini wakati yule shahidi alipokuja, hii hapa, "Mungu aliwaambia, akasema, 'Mngekuwa ...'" Yeye alisema, "Imekuwa ni miezi sita tangu nilipowekewa mikono, na Neno Lako linasema ya kwamba 'Wawekee mikono wagonjwa, nao watapata afya.' Nami niliwekewa mikono na mmoja wa watumishi Wako waliotiwa mafuta, nami sijapona bado. Kwa hivyo Wewe ni mwenye kujifanya wa uongo, kwa maana Neno Lako halimaanishi lisemavyo."

94 Kwa hiyo ushuhuda ulipokuja, wa kweli ulikuwa ni huu, ya kwamba "Neno Lake ni kweli. Yeye kamwe hakusema ni lini angefanya jambo hilo, alisema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.' Mnaona? Mnaona, hivyo ndivyo alivyosema, 'Watapata afya.' Kwa hivyo kama ni muujiza wa mwelekeo kama huu ambao umetendeka hivyo tu au ni kumtii tu Mungu, hiyo ni juu Yake katika mtu binafsi. Mnaona? Lakini kama mtu binafsi akiliamini, sijali itachukua muda gani. Yeye alimwambia Ibrahimu, 'Utapata mtoto kwa Sara.' Mtoto mchanga hakuja kwa miaka ishirini na mitano. Alimwambia Nuhu itanyesha. Nuhu akawa na gharika ... safina—safina iliyojengwa kwa ajili ya gharika, miaka mingi, mingi kabla ya gharika kuja, lakini alijua itanyesha. Biblia ilisema, 'Kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule na Mungu atamwinua.'" Lini? Yeye hakusema. Mungu ni mwenye haki, Yeye ni wa kweli, soma tu kile Neno Lake linachosema."

Hivyo ndivyo nimefanya usiku wa leo, kuwawekea mikono wagonjwa. Sasa, ninaamini kila mmoja wao ataponywa. Ninaamini, kila mmoja wao. Mnaamini vivyo hivyo? Sasa amini kwa ajili ya watu hawa wanaoteseka.

95 Kuna bibi mdogo hapa, inaonekana kana kwamba ninapaswa kujua, nilimwomba jana usiku, huko nje kwenye mstari wa maombi. Jina lake ni nani? Chambers ... Chambless. Kama maskini bibi huyo angeishi—angaliishi kawaida, asingepata mateso, hakika alikuwa ni mwanamke mrembo. Naye ameketi pale sasa, akitetemeka. Roho ya kupendeza, nzuri katika msichana huyo. Naye ameketi pale akishtuka-shtuka hivi. Loo, jinsi jambo hilo linavyouvuja moyo wangu. Namna ambavyo nimetamani ... jinsi tu ningependa!

Huyu hapa mtoto mchanga, mama ameketi hapa amemshika. Ulimi wake mdogo ukining'inia nje, mwili wake mdogo unateseka. Vipi kama huyo alikuwa ni mtoto wangu Joseph? Vipi kama alikuwa ni mjukuu wangu mdogo Paul? Vipi kama huyo alikuwa Rebeka ameketi kule nyuma, ama Sara? Vipi kama Bibi

Simpson hapa alikuwa ni mke wangu Meda? Huyu kijana anayeketi hapa alikuwa ni Billy Paul? Huyu mwanamke mzee anayeketi hapa alikuwa ni mama yangu? Kumbuka, ni mtoto wa mtu fulani, dada wa mtu fulani, binti ya mtu fulani, na mwana wa mtu fulani. Mnaona? Mimi ni ndugu yao, Yeye ni Mwokozi wetu. Yote niwezayo kufanya ni ... imani niliyo nayo inatolewa kwa niaba yao. Hayo tu ndiyo ninayojua.

96 Sasa, Bwana anaweza kunionyesha ono, angeweza kuniambia shida ya kila mmoja wao. Ninaweza kuthibitisha jambo hilo kwenu, mnaona, mnajua jambo hilo. Lakini hilo haliwaponyi. Hilo haliwaponyi. La, haina budi kuwa ni kitu kinachodondoka ndani yao, mnaona. Nami natumaini ...

Kama vile ningeweza kwenda hapa kumchukua kila mmoja wenu na kuwabatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo, hilo halitawaondolea dhambi zenu. La, la! La, siamini katika ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo kwa kuzaliwa mara ya pili; naamini Damu ndiyo inaleta kuzaliwa mara ya pili, mwaona, si kule majini. Lakini, mnaona, ningeweza kubatiza na kubatiza, bali unazamishwa tu ukiwa mwenye dhambi mkavu, unakuja mwenye dhambi aliyoloa; mnaona, mpaka utubu kikamilifu. Tubuni, ndipo mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo. Mnaona? Na hapo ndipo ninapotofautiana na harakati za dhehebu la Umoja. Si kubatiza kwa kuzaliwa mara ya pili, la; Ninaamini Damu ndiyo inayosafisha, si maji. Mnaona? *Toba*, na kisha ubatizwe katika Jina la Yesu Kristo.

97 Sasa ninashuka kwenda kuomba. Na watu hawa wako sawa kwako kama walivyo kwangu mimi, labda hata zaidi katika uhusiano huo.

Sasa hebu sote tuungane pamoja, na mikono yenu katika imani, na mkono wangu katika imani, kuishusha mikono ya Bwana Yesu kuiweka juu ya maskini walemavu hawa. Utaomba pamoja nami?

[Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Wale walio na lesu ambazo ni kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka, mnaweza kuzipata mara baada ya ibada. Sasa nisaidie kuwaombea hawa, sivyo?

Mungu, tunakushukuru, Bwana, kwa yale uliyofanya usiku wa leo. Tunakushukuru kimbele kwa ajili ya uponyaji wa kila mtu aliyepitia kwenye mstari. Mungu mpenzi, ninaomba juu ya lesu hizi, labda kwa ajili ya wengine ambao hata hawangeweza kuja mkutanoni, na wapendwa wao walileta lesu. Katika Biblia tunafundishwa ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo, lesu au nguo. Sasa, hao watu kule nyuma walikuwa wameishi mbele Zako, walikuwa wamekuona Wewe barabarani, walikuwa wamekuona Wewe katika mkutano wao, nao walikuwa wamemwona Roho Wako yule yule juu ya Paulo. Nao walijua haikuwa mtu huyo, ilikuwa ni Roho Wako aliyekuwa akiyatawala maisha yake, kwa kuwa tunamwona Paulo akifanya mambo yale yale uliyofanya.

Na sasa, Bwana, watu wa siku hizi wanamwona Mungu yule yule akiishi katika Kanisa Lake pamoja na watu Wake. Nao wameleta lesu hizi, wapate kuzichukua tokea hapa kwenda kwa wapendwa wao. Jalia, Mungu, ya kwamba kila mmoja wao ataponywa kwa njia Yako mwenyewe. Hatuombi jambo lo lote lifanywe kwa njia yo yote au tabia yo yote; tunaomba tu, "Kwa njia Yako mwenyewe, Baba, waponye." Kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ninatoa ombi hili la imani juu yake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

98 Nimekuwa na wakati mzuri sana wa ushirika karibu na imani yako, uwepo wako katika Yesu Kristo. Huu utakuwa ni mkutano ambao nitaukumbuka kwa muda mrefu juu ya yale yaliyotukia: upendo, kushirikiana, ushirika.

Na sasa, mpaka tutakapokutana tena, Mungu wa Mbinguni na awaongoze. Yeye ambaye huzifanya nyota ziangaze sana usiku kuangazia njia wakati kuwa giza, na aiweke nuru kwa Nyota ya Bethlehemu ili ikuongoze kwenye maisha kamili ya kujitolea katika Neno Lake, ndilo ombi langu.

Hata twonane, hata twonane,  
Hata tutakapokutana miguuni pa Yesu;  
Hata twonane, hata twonane,  
Mungu awe pamoja nanyi daima.

Sasa hebu na tusimame. *Imani Yangu Inakuangalia Wewe! ...?...* Mimi ... vema, nitabadilisha jambo hilo. Ninaamini hilo ni sawa. (Samahani.)

Imani yangu inakuangalia Wewe,  
Ewe Mwana -Kondoo wa Kalvari,  
Mwokozi wa Kiungu!  
Sasa nisikie ninapoomba,  
Ondoa dhambi zangu zote,  
Ee, hebu niache tangu leo  
Kuwa Wako kabisa!

99 Sasa hebu na tupeane mikono tunapoimba.  
Wakati ninapopitia maisha yenye utata gizani,  
Na majonzi yakiwa yamenizunguka  
Wewe uwe Mlinzi wangu;

Amuru giza ligeuke kuwa mchana,  
Futa machozi ya huzuni,  
Wala usiniache nipotee  
Kutoka Kwako kando.

Unajisikia vizuri sasa, sivyo?

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
Ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua.  
Sasa juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
Ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua.

Huo ndio ujumbe wetu wa kufunga kampeni hii.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
Ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua.

100 Tuinamishe vichwa vyetu. Huku magurudumu yakivumisha wimbo kuelekea nyumbani, natumaini ita... mngesikia mvumo wa magurudumu, kunguruma kwa mtambo:

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,  
Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
Ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha kibwagizo — Mh.]  
... Hua,  
Mungu hutuma upendo Wake safi, mtamu,  
Ishara kutoka juu,  
Juu ya mbawa za hua.

Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nawapa ... Ndugu Noel.



[www.messagehub.info](http://www.messagehub.info)

Mahubiri Na  
**William Marrion Branham**  
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7